Fuatilia Pesa

Mwongozo wa Mafunzo juu ya Kufuatilia Matumizi ya Mali ya Umma

Umeandaliwa na:
Hakikazi Catalyst
REPOA
TGNP

Kimehaririwa na kuchapishwa Policy Forum

Fuatilia Pesa

Mwongozo wa Mafunzo juu ya Kufuatilia Matumizi ya Mali ya Umma

Umeandaliwa na:
Hakikazi Catalyst
REPOA
TGNP

Kimehaririwa na kuchapishwa Policy Forum

Kimehaririwa na kuchapishwa na Kikundi Kazi cha Serikali za Mitaa cha Policy Forum

© Policy Forum 2007

Yaliyomo

Vifupisho 6
SEHEMU YA 1: Utangulizi 7
1.1 Malengo ya Mwongozo Huu 7
1.2 Mlengwa wa Mwongozo huu 7
1.3 Mtazamo wa mwanzo: kujenga mazingira ya kufaidisha washiriki wote 8
1.4 Jinsi ya Kutumia Mwongozo Huu 9

Kipengele A: Taarifa za Awali juu ya Kazi za PETS 11

SEHEMU YA 2: PETS ni nini na ina umuhimu gani? 12
2.1 Utangulizi: Umuhimu wa Taarifa za Kifedha 12
2.2 PETS na Taarifa za Kifedha 13
2.3 Umuhimu wa PETS 15
2.4 Baadhi ya vikwazo/ matatizo katika utekelezaji wa PETS 16

SEHEMU YA 3: Kuanzisha PETS: Mawazo ya Msingi na Methodolojia 18
3.1 Utangulizi 18
3.2 Dhana ya Msingi: Ni kwa njia ipi bajeti yaweza kutoegemea upande wowote? 18
3.3 Watendaji Wakuu na Washirika 19
3.4 Muhtasari wa Muundo wa Kuanzisha PETS 20

SEHEMU YA 4: Stahili na Haki - Msingi wa Kisheria na Kifedha wa PETS 23
4.1 Haki 23
4.2 Haki, Uwazi na Upatikanaji wa Taarifa 25
4.3 Haki ya Taarifa za Fedha: Msingi wa Uwazi katika Tawala za Mitaa 26

SEHEMU YA 5: Mipango na Bajeti Ngazi ya Wilaya 29
5.1 Kuelewa namna ya Kuandaa Bajeti ya Wilaya 29
5.2 Vyanzo vya Taarifa za PETS 30
5.3 Taarifa za Ugavi 32
5.4 Mifano Mitatu ya Matokeo ya PETS 33

Kipengele B: Mitazamo ya Kukamilishana katika Utekelezaji wa PETS 39

SEHEMU YA 6: MTAZAMO WA KWANZA: Kufanya PETS ihudumie makundi yaliyotengwa na jamii 40
6.1 Hatua ya Kwanza: Kuhakikisha kwamba dhana za msingi zinaeleweka 40
6.2 Zana za Kuuboreshea Mtazamo wa Kwanza 42

SEHEMU YA 7: MTAZAMO WA PILI 46
7.1 Utangulizi 46
7.2 PIMA Card nini? 46
7.3 PIMA Cards zaweza kutumiwaje? 48
7.4 Umuhimu wa PIMA Cards 48
7.5 Vichocheo vya mafanikio ya PIMA Cards 49
7.6 Mchakato wa PIMA Card 50
7.7 Shughuli za PIMA Cards: Hatua kwa Hatua 50
7.8 Nyenzo maalum na Mazoezi ya Kufundishia 53

SEHEMU YA 8: Hitimisho 57
8.1 kutoka kujenga mifumo hadi kufanya mabadiliko hasa yapatikane 57
8.2 Habari za nyongeza 57
Kiambatisho 1: Vyanzo zaidi vya Kujisomea 58
Kiambatisho 2: Fomu tupu ya PETS 59

Vifupisho

LAAC - Kamati ya Ukaguzi wa Mahesabu ya Serikali za Mitaa

LGA - Mamlaka ya Serikali za Mitaa

MDA -Wizara, Idara na Wakala

O&OD - Vikwazo na Mianya ya Maendeleo

PER - Marejeo ya Matumizi ya Mali za Umma

PET - Ufuatiliaji wa Matumizi ya Mali za Umma

PETS - Muundo wa Kufuatilia Matumizi ya Mali za Umma (katika machapisho mengine hii pia huitwa 'Stadi za Ufuatiliaji wa Matumizi ya Mali za Umma)

OWM - Ofisi ya Waziri Mkuu

TAMISEMI -Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

JMT- Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

PMSM - Programu ya Mabadiliko ya Serikali za Mitaa

SEHEMU YA KWANZA: Utangulizi

Ufuatiliaji wa Matumizi ya Mali za Umma (PETS) ni kufuatilia fedha tangu inapotolewa na serikali kuu, mpaka mikononi mwa serikali za mitaa na hatimaye kwa watumiaji wa mwisho, kama vile mashule na kliniki.

Mwongozo huu hutoa msaada wa aina tofauti tofauti jinsi PETS inavyoweza kutekelezwa. Umeandaliwa ukitilia maanani kwamba wewe msomaji una maarifa ya msingi juu ya bajeti na jinsi zifanyavyo kazi, na pia kwamba una shauku ya kuendeleza uwazi na uwajibikaji zaidi juu ya masuala yahusuyo bajeti za serikali.

Mwongozo huu umetokana na ushirikiano wa Hakikazi Catalyst, REPOA na Mtandao wa Masuala ya Jinsia (TGNP). Kila moja ya makundi haya ya kijamii limekuwa likifanya kazi peke yake, lakini hapa yamefanya kazi kwa pamoja kama wanachama wa baraza la sera la mashirika yasiyo ya kiserikali, (yaani NGO Policy Forum), juu ya masuala ya bajeti na PETS. Yameamua kufanya kazi safari hii ili kuweza kuuleta uzoefu wao pamoja. Kwa msaada wa Mfuko wa Elimu wa Jumuiya ya Madola na Taasisi ya Jumuiya za Kiraia (Foundation for Civil Society), mwongozo huu utafanyiwa majaribio katika wilaya tofauti tofauti kuanzia Septemba 2006. Baada ya hapo utafanyiwa marejeo ili kuingiza mitazamo mipya tutakayokuwa tumejifunza, ili hatimaye tuweze kutoa mwongozo ulio bora zaidi utakaosaidia kukuza utendaji wa shughuli za PETS.

1.1 Malengo ya Mwongozo Huu

Malengo ya msingi ya mwongozo huu ni:

- Kuongeza uelewa juu ya PETS na jinsi ya kuitumia katika kutengeneza bajeti kwa mtazamo unaozingatia zaidi hali ya umasikini na masuala ya jinsia.
- Kutoa maarifa, ujuzi na mbinu za kufuatilia mchango (vyanzo), utekelezaji na matokeo ya bajeti.
- Kukuza uwazi na uwajibikaji wa serikali za mitaa.
- Kujenga uwezo wa mashirika ya kiraia kusaidia kuweka vipaumbele kwenye bajeti ili kulenga mahitaji ya wanawake masikini, wanaume masikini, wasichana, wavulana na makundi mengine yaliyosahauliwa na jamii.

1.2 Mlengwa wa Mwongozo huu

Mwongozo huu umeandaliwa mahsusi kwa ajili ya makundi makuu matatu:

- Maafisa wa serikali za mitaa na madiwani
- Mashirika ya kiraia ngazi za wilaya
- Waandishi wa habari

Mwongozo huu umeandaliwa kwa dhana kwamba msomaji una maarifa kiasi juu ya bajeti, na pia kwamba una mawazo ya msingi juu ya masuala ya jinsia. Mwongozo huu unachukulia pia kwamba msomaji una msimamo thabiti juu ya utawala bora na ukuzaji wa uwazi na uwajibikaji kwa wananchi katika nyanja zote.

1.3 Mtazamo wa mwanzo: kujenga mazingira ya kufaidisha washiriki wote

Hapa tutaongelea mitazamo ya jinsi ya kuleta maendeleo chanya kwa kushughulikia matumizi ya mali ya umma, ambako kunaweza kuhusisha walau moja ya mambo yafuatayo:

1. Kubainisha na kutatua matatizo:

   Kuliweka tatizo kwenye ajenda, kulitolea suluhisho na kutafuta uungaji mkono katika ufuatiliaji.

2. Kushawishi mitazamo ya jamii:

   Mchakato mahsusi wa kuathiri mitazamo ya jamii.

3. Kushawishi sera za serikali:

   Kulenga kubadili sera na programu za serikali, taasisi na mashirika.

4. Kukuza demokrasia:

   Mchakato wa mabadiliko ya kijamii kuathiri fikira (mitazamo), mahusiano ya kijamii na mahusiano ya kimamlaka, ambayo huimarisha makundi ya kijamii na kukuza zaidi demokrasia.

Majadiliano na Tafakari:

Uanzapo kutafakari juu ya PETS na kushirikiana na mashirika yasiyo ya kiserikali, maafisa wa serikali za mitaa na madiwani kuanzisha PETS, zingatia yafuatayo:

Ni fasili ipi inakaribia zaidi na kile unachotaka kufanikisha? Kuna chochote ambacho ungependa kuongeza?

Je, hicho ndicho kila mmoja wenu anachovutiwa nacho? Mnawezaje kutafuta muafaka na kujenga lengo

Mtazamo uliotumiwa hapa hujulikana zaidi kama "constructive engagement", yaani mtazamo wa miadi saidizi katika ushawishi. Mtazamo huu hulenga zaidi hatua za kiufundi na serikali za mitaa kuliko hatua za juu za kisiasa, japokuwa uungwaji mkono wa kisiasa tayari umeshaanza kupatikana kama itakavyoonyeshwa kipengele 3.3.

Mwongozo hapa unajaribu kushawishi (na hatimaye kuathiri) sera maalum, programu au miradi kwenye ngazi ya wilaya na serikali za mitaa. Ushawishi huu huhusisha kuongea na watu walio na utayari wa kubadilika, lakini pia huhitaji hali ya juu ya maarifa ya kiufundi itokanayo na uzoefu. Hii huwezesha maoni yatolewayo (kama vile masuala ya jinsia au jinsi wazee wachukuliwavyo na jamii) yaweze kutiliwa umaanani. Ushawishi wa namna hii waweza hasa kufanyika sehemu isiyo na umati mkubwa, na huwa ni shirikishi.

Mtazamo huu waweza pia kutumiwa na serikali za wilaya kufanya ushawishi juu ya rasilimali wapokeazo kutoka ngazi ya taifa.

1.4 Jinsi ya Kutumia Mwongozo Huu

Mwongozo huu umegawanywa katika vipengele ambavyo vyaweza kukidhi mahitaji ya watumiaji tofauti tofauti.

1. **Utangulizi**

   Kipengele A: Taarifa za Awali juu ya Kazi za PETS

2. **PETS ni Nini na ina Umuhimu Gani?**

3. **Kuanzisha PETS:** Mawazo ya Msingi na Methodolojia

4. **Haki na Stahili:** Misingi ya Kisheria na Kifedha ya PETS

5. **Mipango na Bajeti Ngazi ya Wilaya**

   Kipengele hiki hutoa nyenzo zifananazo na nyinginezo katika programu yoyote ya mafunzo ya PETS. Kitajikita kwenye muundo wa jumla wa mafunzo ya bajeti unaofuatwa na shirika husika. Vitu vya kujadili vimetolewa mwisho wa kila kipengele. Hivi vyaweza kuingizwa kwenye programu ya mafunzo au kutumiwa tu kukuchangamsha ujisomeapo peke yako.

   Kipengele B: Mitazamo Miwili Ikamilishanayo

6. **Mtazamo wa Kwanza:** Kufanya PETS ihudumie makundi yaliyosahaulika katika jamii – ilenge zaidi kwenye masuala ya jinsia

7. **Mtazamo wa Pili:** Kulenga Kuijengea Jamii Uwezo

   Mitazamo yote miwili ina wazo moja kimsingi, lakini hutofautiana kimsisitizo kama ionekanavyo katika majina yao. Hatua bayana na nyenzo zitumikazo katika mtazamo mmoja zaweza kutumiwa bila tatizo kwenye mtazamo mwingine.

8. **Hitimisho**

Kipengele A
Taarifa za Awali juu ya Kazi za PETS

SEHEMU YA 2: PETS ni nini na ina umuhimu gani?

2.1 Utangulizi: Umuhimu wa Taarifa za Kifedha

Kama ulikwisha jishirikisha kwenye shughuli yoyote ya bajeti, utakuwa unajuwa wazi kwamba kutoa fedha (kutenga na hatimaye kutoa/ kugawa fedha) ndiyo njia rahisi ya kutambua vipaumbele na mipango ya serikali. Kama serikali ikitamka kwamba kutoa maji safi kwa kila wananchi ni moja ya vipaumbele vyake, na wakati huo huo haitengi pesa kusaidia kuongeza ubora wa huduma ya maji, utaamini kipi kati ya kauli na bajeti? Kwa upande mwingine, pale ambapo serikali imedhamiria kubadilika, ushiriki wa wananchi katika masuala ya bajeti unaweza kuimarisha mchakato mzima wa kubadilika.

Mchoro ufuatao huonyesha mzunguko unaoweza kufikiwa, kuanzia kona ya juu kushoto.

Mchoro 1: Kujishughulisha na Mchakato wa Bajeti



Mfumo huu unahitaji watu wajue taarifa halisi za fedha. Mfumo huu una faida mbili: kuboresha mipango na kuboresha uwajibikaji.

1. Kuboresha Mipango

Kwa jumla, pale tu jamii zinapokuwa na taarifa za kifedha na nyinginezo ndipo watu wanapoweza kushiriki katika shughuli za mipango na kushiriki kuleta au kubadili vipaumbele katika wilaya au halmashauri zao.

Bayana zaidi, serikali ya Tanzania imenuia kutekeleza (kwa vitendo) muundo wa O & OD (Vikwazo na Mianya ya Maendeleo) ambao ni methodolojia shirikishi ya kupanga maendeleo. Fungu la Maendeleo kwa ajili ya Serikali za Mitaa (yaani Local Government Capital Development Grants) litatumika kutekeleza mipango ya jamii husika ambayo itakuwa imetokana na methodolojia ya O & OD. Ili mfumo huu ufanye kazi, jamii zinapaswa kuwa na taarifa tofauti tofauti, hasa za kifedha.

2. Kuboresha Uwajibikaji

Mara nyingi serikali za mitaa, madiwani na mashirika yasiyo ya serikali huhitaji kuwafanya wananchi waweze kuwajibika. Miongoni mwa sababu ni:

- Kuwafanya watu watekeleze majukumu yao kama iwapasavyo, kwa ubora, uaminifu na uwazi;
- Kuhakikisha kwamba utekelezaji wa majukumu yaliyopangwa unasimamiwa ipasavyo;
- Kutathmini utendaji dhidi ya malengo au mipango iliyokuwa imewekwa (kwa mfano, ubora wa jengo kulinganisha na mipango iliyokuwa imewekwa);
- Kuhusianisha fedha na matokeo ya kazi (kama vile ubora wa jengo kulinganisha na kiwango cha fedha kilichotumika / kilichopaswa kutumika)

Kudai uwajibikaji hakulengi kujijengea maadui, bali kuwasaidia maafisa wa serikali za mitaa, madiwani na asasi za kijamii kuzielewa barabara huduma ambazo zinagharimiwa kwa fedha ya umma.

Majadiliano na Tafakari

Ukiwa mwanajamii au mshirika katika serikali za mitaa, kwa nini unadhani unahitaji kupata taarifa za kifedha? Orodhesha sababu.

Mchoro ufuatao unaonyesha kwa ufupi faida au umuhimu wa kuwa na taarifa za kifedha.



Umuhimu wa taarifa za kifedha na jinsi unavyotekelezeka vimefafanuliwa zaidi katika kipengele kifuatacho.

2.2 PETS na Taarifa za Kifedha

PETS ni nyenzo za kuwawezesha wananchi kujua jinsi fedha ya serikali inavyotumika. Ni miongoni mwa mbinu nyingi zitumiwazo na mashirika yanayojitahidi kukuza uwazi katika masuala ya bajeti, na pia husaidia kumsha ari ya wananchi kudai

viongozi wawajibike. Fasili rasmi zaidi ya PETS imetolewa katika kisanduku namba 1:

Kisanduku namba 1: Fasili ya PETS

PETS ni mfumo wa kutoa taarifa za mambo ya fedha kwa jinsi inayowawezesha wahusika (watendaji) tofauti tofauti kujadili vyanzo na matumizi ya fedha. Huwawezesha walengwa kulinganisha fedha iliyoingia na matumizi yaliyofanyika. Huwawezesha maafisa na wananchi wa kawaida kuelewa vema zaidi stahili zao katika bajeti, na pia kuwawezesha kuona kama kweli fedha ya umma inatumiwa kwa jinsi iliyokuwa imepangwa kwenye bajeti. PETS inatarajiwa kufuatilia mtiririko wa fedha katika ngazi tofauti za serikali ili kubaini kiasi cha fedha kilichotengwa hufika kila hatua, na hatimaye ni kiasi kipi humfikia mlengwa wa mwisho kama vile mtoto wa shule, mgonjwa au mtu anayehitaji kuwahudumia hawa, yaani mwalimu na muuguzi, afisa kilimo nk.

PETS zimetokana na uzoefu katika stadi za ufuatiliaji wa matumizi ya mali ya umma. Kwa miaka mingi stadi za ufuatiliaji zimekuwa zikitumika katika nchi tofauti kufuatilia kwa karibu kiwango cha fedha kitolewacho na ngazi za juu za serikali, hadi wizarani, idarani, wakala (MDA) na hatimaye kumfikia mlengwa wa mwisho. PETS zimefanikiwa sana kuonyesha kama fedha inafika ilikolengwa kwenda, na pia kama inatumiwa kutekeleza majukumu yaliyokusudiwa. Mfano ni kuangalia kama fedha ya kujenga madarasa inafika mashuleni, au vile vile kama kutumia fedha kuboresha madarasa pekee kwaweza kuboresha mahudhurio ya wanafunzi na kuinua kiwango cha elimu.

Mbali na faida hizi, PETS zina mapungufu yafuatayo[1]:

Zaweza kuwa ngumu kwa mashirika ya kijamii kutekeleza kwa kuwa wakati mwingine si rahisi kupata taarifa sahihi za kifedha. Hii husababishwa na mtazamo potofu kuwa PETS zinalenga kudhibiti maafisa wa serikali.

Zinafanikiwa zaidi pale zinapotumiwa na watendaji wa nje, kama vile serikali au wafadhili wanapoingia mapatano na taasisi ya uchunguzi kufanya stadi hizi kwa niaba, ambapo viongozi husika wanalazimika kuandaa taarifa zinayohitajika. Hata hivyo, hii huwafanya viongozi hawa wawajibike kwa walio juu yao (wafadhili ama serikali) kuliko kuwashirikisha wananchi katika masuala ya bajeti.

Mpaka sasa stadi hizi zimekuwa zikifanywa mara moja tu (bila kurudiwa tena), na zimekuwa hazitoi mafanikio ya muda mrefu.



Katika mwongozo huu PETS zinalengwa kwenda mbali zaidi ya kuwa tu mfumo wa kufuatilia matumizi ya mali ya umma. Zinalengwa kuwa miundo inayoweza kuendelezwa na kuendelea kufanya kazi daima. Ili PETS ziendelee zinahitaji kuwapo na taarifa zisizokoma kutoka serikalini kwenda kwa mashirika ya kijamii na jamii nzima juu ya fedha zinavyotumiwa, kama ionyeshavyo kwenye mchoro ufuatao.

Tunataraji kwamba hii itawatia moyo watu kujishirikisha zaidi katika mijadala juu vipaumbele katika matumizi, na hatimaye kuamua jinsi rasilimali zinavyoweza kutumiwa ili kuhudumia mahitaji ya makundi yaliyosahauliwa kijamii.

Miundo yaweza kuwa rahisi sana, au migumu sana kutegemea na unacholenga kufanikisha. Waweza kufuatilia sekta moja tu kutoka ngazi moja hadi nyingine ya serikali; kwa mfano, sekta ya kilimo kuanzia ngazi ya wilaya hadi kijiji. Au waweza kufuatilia sekta zaidi ya moja ukianzia serikali kuu hadi ngazi ya kijiji.

Kingine kinachofanya PETS kuwa za pekee ni kwamba katika utekelezaji wake maafisa wa wilaya au halmashauri hushirikiana na mashirika ya kijamii. Maafisa wamekuwa wakitoa taarifa za kifedha na nyinginezo kwa vipindi maalum kama vile mwaka au miezi mitatu mitatu. Siku za nyuma ilikuwa ngumu kiasi kufanikisha PETS namna hii, lakini baada ya serikali kutoa Plan Rep2 na Epicor, utoaji wa taarifa unatarajiwa kuwa rahisi zaidi.

2.3 Umuhimu wa PETS

PETS zina faida nyingi. Husaidia watu kupata taarifa za masuala ya kifedha, na kuwawezesha kuelewa uhusiano kati ya huduma zitolewazo, mgawo wa fedha kwenye bajeti, na matumizi halisi. Ufuatao ni muhtasari wa uzoefu katika PETS.

Taarifa zitokanazo na PETS zaweza kuwa na faida kwa watendaji tofauti tofauti kama ifuatavyo:

Kwa wanaotaka kujua endapo kuna mapungufu katika mfumo

Hii yaweza kufanyika kwa kulinganisha fedha halisi iliyotolewa serikali kuu na kiasi kilichopokelewa ngazi za wilaya na kijiji[2]. PETS zinaweza kubaini kiwango cha mapungufu na ngazi yalipotokea mapungufu hayo.

Kwa wanaotaka kuelewa chanzo cha matatizo

Kwa mfano, kama hakuna dawa za kutosha kliniki, ni kwa nini? Je, ni kwa ajili ya upungufu wa fedha kwenye bajeti? Au je, fedha haikutolewa kama ilivyostahili? Je, matatizo yalijitokeza kwenye manunuzi ya vifaa? Au labda matatizo yalikuwa kwenye ugawaji wa vifaa/zana?

Kwa wale wanaotaka kujuwa sababu za halmashauri kutotekeleza mipango au ahadi

Kwa mfano, kama ilitolewa ahadi ya kuboresha barabara, na mabadiliko yoyote hayaonekani, sababu yaweza kuwa ipi? Moja ya sababu yaweza kuwa kwamba pesa haijatoka serikali kuu kwa kiwango kilichotarajiwa. Kwa mfano, kama kwenye bajeti kulikuwa kumepangwa shilingi milioni 20 halafu zikatolewa shilingi milioni 15 tu, yaweza kuwa vigumu kutekeleza ahadi na mipango yote. Katika hali kama hii PETS ndizo zinazoweza kuonyesha picha halisi ya mambo na kuwawezesha wadau wote kuona tatizo lilipo.

Kwa wale wanaotaka kuthibitisha ulinganifu katika matumizi ya fedha

Hii hufanywa kwa kulinganisha kiasi cha fedha kilichotumika na matokeo ya matumizi husika. Kwa mfano, ikisemwa kwamba shilingi milioni 10 zimetumika kujenga zahanati, wananchi wanaweza kuangalia na kujiuliza kama zahanati wanayoiona yaweza kuwa kweli imejengwa kwa thamani iliyotajwa, yaani milioni 10. Huu waweza kuwa ndiyo mwanzo wa kuwahoji maafisa na wengine wote walioshiriki katika mradi huu wa kujenga zahanati.

Kwa wale wanaotaka fedha itumike vema ili kupata mafanikio zaidi Kwa mfano, katika juhudi za kuwezesha wanafunzi wengi zaidi kupata kisomo, yawezekana kujiuliza kama kuwapa wanafunzi chakula cha mchana shuleni kwaweza kuleta mafanikio bora zaidi kwenye elimu kuliko kujenga vyumba zaidi vya madarasa.

PETS yaweza pia kusaidia kutoa taarifa sahihi na za kina. Hii hufanyika kwa kutumia njia zaidi ya moja ya kukusanya taarifa. Hii humaanisha pia kukusanya taarifa kutoka vyanzo mbalimbali, na ngazi tofauti tofauti kama vile ngazi ya vijiji na hata wilaya.

Kwa ufupi, PETS hutoa njia mbadala ya kuyatazama matokeo ya kazi sambamba na matendo ya watoa huduma. Hii yaweza kusaidia kuwapa taarifa (na hata mtazamo) mpya watungaji wa sera na wengineo.

2.4 Baadhi ya vikwazo/ matatizo katika utekelezaji wa PETS

Mbali na kwamba PETS ni muhimu sana, ni ngumu kiasi kuzitekeleza. Baadhi ya matatizo au vikwazo ni kama ifuatavyo:

Kupata taarifa sahihi yaweza kuwa vigumu. Kwa mfano, mahesabu ya fedha ngazi ya wilaya huwa yamewekwa pamoja kwa muundo ambao si rahisi asiyehusika kufuatilia fedha ielekeavyo kwenye ngazi za kata na vijiji. Mbali na ugumu huu, baadhi ya njia za kutatua tatizo hili zitajadiliwa katika kipengele cha 4.

Fedha itokapo kwenye vyanzo vingi tofauti ufuatiliaji waweza kuwa mgumu zaidi. Baadhi ya taasisi na watu wenye nguvu ya kifedha wasingependa baadhi ya maafisa wawajibishwe, au wasingependa kuzijengea jamii husika uwezo. Hii yaweza kusababisha matatizo mengi, ikiwamo kuzuia baadhi ya taarifa muhimu (kwa kufanya zisipatikane kirahisi), ambayo pia yaweza kuwafanya wananchi washindwe kuhoji mambo ya msingi. Ubanaji wa namna hii hufanya miundo iliyopo iendelee bila kubadilishwa kuendana na matakwa ya jamii. Hii inajulikana kama 'elite capture'. Endapo mtu au kundi linaonekana kama linaziunga mkono PETS wakati ukweli ni kwamba linajenga vikwazo dhidi ya PETS, hali hii hujulikana kama 'illegitimate representation' au uwakilishi haramu.

Hata hivyo, mitazamo iliyoelezewa humu kuhusu utekelezaji wa PETS hutoa mwanya wa wadau mbalimbali kujishirikisha moja kwa moja na kuwa sehemu ya mfumo imara. Hii inawezesha wadau wote kuwa na uhakika wa kupata habari.

SEHEMU YA 3: Kuanzisha PETS: Mawazo ya Msingi na Methodolojia

3.1 Utangulizi

Lengo la PETS ni kuwezesha umma kupata taarifa za masuala ya fedha kirahisi na katika muundo unaoweza kueleweka kirahisi. Kwa sasa kuna taarifa aina tofauti tofauti za masuala ya kifedha (tazama kisanduku namba 4), lakini taarifa hizi si rahisi kueleweka kwa baadhi ya wananchi. Mara nyingine taarifa hizi huwa zinaandaliwa kwa ajili ya wadau tofauti tofauti kwa malengo tofauti tofauti; wakati mwingine taarifa hazipewi nafasi sawa katika kutangazwa/ kuenezwa.

Vyanzo vya Taarifa za Kifedha

Kuna njia tofauti ambazo wananchi wa kawaida wanaweza kuzitumia kupata taarifa za kifedha ngazi ya wilaya. Hizi ni pamoja na:

- Taarifa asilia za kifedha, yaani taarifa za mapato, mizania (balance sheet) na taarifa ya matumizi ya fedha,
- Utoaji wa mara kwa mara wa taarifa juu ya fedha iliyopokelewa,
- Magazeti yaeneayo nchi nzima kama vile Nipashe, Majira, nk.

Zifuatazo ni sifa za msingi za PETS:

Ushirikishaji: Japokuwa PETS ni juhudi za wananchi katika jamii zao, inatarajiwa kwamba PETS zitaendelezwa kwa kushirikiana na mashirika ya kijamii, OWM-TAMISEMI na mamlaka za serikali za mitaa. TAMISEMI watatoa barua za utambulisho na misaada mingineyo itakayowezesha ushirikiano kati ya PETS na serikali za mitaa. Yatarajiwa pia kuwa vitakuwapo vikao vya mashauriano baina ya mashirika ya kijamii na mamlaka za wilaya, na kuyaalika mashirika ya kijamii kuhudhuria vikao vya kamati ya fedha.

Kuanza pole pole na kwa uangalifu: Kwa kuanzia, PETS zitalenga tu kuonyesha mtiririko wa sasa wa mali na kujaribu kuonyesha jinsi fedha itumikavyo. Hii itahusisha pia kupata jumla kuu, yaani kujumlisha fedha kutoka vyanzo tofauti vya fedha. Baada ya wahusika kushirikishwa kupata na kuzitumia taarifa hizi, yaweza kuwa rahisi sasa kufuatilia na kukusanya taarifa maalum zaidi.

Kurahisisha taarifa: Ni vema kutoa taarifa kwa njia iliyo rahisi kueleweka ili kuzisaidia mamlaka za serikali za mitaa. Ili kufanikisha hili, tayari kuna juhudi mahsusi kutumia PlanRep ili kutengeneza taarifa rahisi.

Kusaidia badala ya kukagua: Kazi hii hailengwi kuwa ukaguzi wa matumizi, bali kuuwezesha umma kujua fedha iingizwayo wilayani, na kuwawezesha kuelewa vema masuala ya bajeti na matumizi. Hii yaweza kuzisaidia halmashauri kudhibiti matumizi ya fedha na kuandaa bajeti kwa upeo mkubwa zaidi.

3.2 Dhana ya Msingi: Ni kwa njia ipi bajeti yaweza kutoegemea upande wowote?

Kinadharia, bajeti huonekana kuwa chombo cha sera kisichoegemea au kupendelea upande wowote, ambacho hunyambulisha jumla za mapato na matumizi ya serikali.

Hata hivyo, bajeti haiko huru kiasi cha kutoegemea pande fulani fulani za jamii. Katika hali halisi bajeti huashiria maamuzi juu ya stahili za makundi tofauti tofauti katika jamii moja: kwa mfano, nani atozwe kodi, nani asamehewe kodi, huduma zipi ziwe bure, nani apate huduma za bure na kadhalika. Pia mara kwa mara bajeti zimekuwa hazizingatii majukumu tofauti ya wanaume na wanawake katika jamii, au hata uwezo wao.

Hata pale ambapo fedha inatengwa kwa msingi wa maamuzi yanayowagusa wadau wote, fedha imekuwa haitolewi kulingana au kufuatana na maamuzi yenyewe. Kwa maneno mengine ni kwamba kutenga fedha na kugawa fedha vimekuwa haviendani.

3.3 Watendaji Wakuu na Washirika

3.3.1 Madiwani

Madiwani wanaweza kuvutiwa na uanzishwaji wa PETS kwa sababu wao ndiyo wawakilishi wa wananchi ngazi ya wilaya, na wanahitaji maarifa zaidi juu ya masuala ya fedha ili waweze kuzihoji mamlaka husika na hatimaye kuwaeleza kwa kina wananchi waliowachagua hali halisi ya huduma zitolewazo.

Hata hivyo madiwani wanaweza kukosa muda kujifunza PETS, au wanaweza kupungukiwa maarifa ya masuala ya kifedha. Kwa upande mwingine, wanaweza kudhani kwamba wanajua masuala ya kifedha vya kutosha kwa kuwa wamekuwa wakipokea taarifa za mara kwa mara ambazo huzijadili kwenye vikao vya halmashauri.

3.3.2 Maafisa wa Wilaya

Hawa nao wanaweza kuvutwa na uanzishaji wa PETS kwa kuwa wanahitaji kuelewa kwa hakika jinsi rasilimali zitumikavyo katika utoaji wa huduma. Hii yaweza kuwasaidia kuboresha masuala ya kutenga na kudhibiti rasilimali.

Lakini maafisa hawa pia wanaweza kushindwa kuzifanikisha PETS kwa sababu kama za madiwani. Mbali na kukosa muda, wao wana ajira na majukumu ya kudumu (tofauti na madiwani). Yawezekana pia kwamba kutenga na kudhibiti rasilimali si miongoni mwa vipaumbele vyao.

3.3.3 Jamii zipokeazo huduma

Jamii zipatazo huduma kutoka wilayani zaweza kuanzisha na kuendesha PETS ili kuboresha viwango vya huduma wanazopokea. Hii yaweza kufanywa kwa kukadiria ubora wa huduma ukilinganishwa na rasilimali (fedha nk) walizotengewa kwa huduma hizi. Wanaweza pia kutaka kuwawajibisha viongozi wao juu ya matumizi ya rasilimali na pia kupanga upya vipaumbele katika matumizi ya rasilimali.

Wakati inatarajiwa kwamba jamii ndizo zinaweza kufaidika sana na PETS, ndizo zenye nafasi ndogo zaidi ya kutekeleza PETS. Kuanzisha na kuendesha PETS kunahitaji muda na utaalamu, na pia kujiandaa kifikra kwamba ni haki na jukumu kuhoji juu ya mapato na matumizi ya mali ya umma. Kwa hiyo unahitaji kujiandaa vema na kuwa na uthubutu wa kutosha kufuatilia taarifa kutoka kwa viongozi na maafisa wa wilaya. Unahitaji pia kuwa na muda wa kutosha kuzichunguza kwa undani taarifa ulizopata, kisha uwe na ari ya kuchukua hatua kutokana na

ulichobaini kwenye taarifa. Kwa hali hii jamii zinahitaji msaada mkubwa sana ili kutekeleza PETS.

3.3.4 Mashirika ya Kijamii (CSO)

Mashirika ya kijamii ni mwenza katika utekelezaji wa PETS. Hamu yao yaweza kutokana na nia yao ya kuboresha maisha ya wanajamii yanakofanyia kazi. Faida mashirika haya yaliyonayo kulinganishwa na washirika wengine waliotajwa kwenye vipengele vilivyotangulia ni mpangilio wao safi wa kuweza kutekeleza PETS. Mashirika yaweza kutenga muda ili kuzitafuta taarifa za masuala ya fedha, kuzichanganua na hatimaye kueneza matokeo ya taarifa hizi kwa wadau. Shirika laweza kuwa na shughuli zake sehemu kubwa ya wilaya, hali iwezeshayo taarifa kuenezwa kwa njia rahisi na kwa fedha kidogo. chini huonyesha jinsi mashirika ya kijamii yanavyoweza kusaidia kukuza uwazi na uwajibikaji katika masuala ya kifedha.

Hata maelekezo ya serikali huonyesha kwamba mashirika yana nafasi nzuri zaidi ya kutekeleza PETS (tazama kipengele 4.3.3).

Mchoro ulioko kipengele 2.2 huonyesha uhusiano imara wa kiutendaji miongoni mwa watendaji tofauti tofauti ili kuhakikisha kwamba mchakato mzima wa kushirikishana katika kupanga na kutengeneza bajeti unafanya kazi sawa kwa wadau wote.

3.4 Muhtasari wa Muundo wa Kuanzisha PETS

HATUA YA 1: Fanya mapitio, kuanzia ngazi ya taifa

- Chambua sera na malengo ya kitaifa, ukiangalia hasa makundi, masuala au sekta zinazokuhusu zaidi. Usisahau kugusia suala la jinsia katika hatua hii.
- Chunguza mapitio ya matumizi ya mali ya umma (PER) ili kupata utambuzi juu ya mchakato wa bajeti.
- Chambua na kutathmini malengo ya wilaya yanavyoendana na sera na malengo ya kitaifa, na uone jinsi yanavyoweza kukuathiri.

HATUA YA 2: Pata picha ya uandaaji wa bajeti katika ngazi ya wilaya

Namna nzuri ya kufanya hivyo ni kufikiri katika misingi ya Uwezo, Udhaifu, Fursa na Vitisho (maarufu kwa Kiingereza kama SWOT) ili kuweza kujibu maswali yafuatayo:

- Nani hushiriki? (wanawake, wanaume, vijana wa kiume na wa kike, watu wenye ulemavu, watu waishio na VVU, wachungaji n.k.)
- Hushiriki kwa namna gani?
- Ni mitazamo au sauti za nani husikilizwa vizuri zaidi?
- Ufuatiliaji wa mbinu ya **O&OD** (Vikwazo na Mianya ya Maendeleo) na namna inavyotumika katika wilaya husika. Je kuna vipaumbele vitokanavyo na kazi hii?

HATUA YA 3: Ongea na watendaji muhimu kuhusu PETS na manufaa yake kwao.

Hii ni aina ya ushawishi inayojumuisha kuongea na watu ambao wanaweza kuruhusu mabadiliko, lakini ni muhimu sana kuzingatia ufahamu wa hali ya juu utokanao na uzoefu wa kiutendaji (kama vile uelewa juu ya masuala ya jinsia, watoto wa mitaani n.k.). Unahitaji kulenga kundi maalum, na kutumia muda kujenga mahusiano mazuri nao. Fikiria walengwa kwa misingi ya watu binafsi na siyo asasi kama "Halmashauri za Wilaya". Wachunguze watu hao kwa kina juu ya madhumuni, malengo na mipango yao. Waainishe hao watu kama walengwa wako wa msingi, na jitahidi kuwashawishi.

Fikiria pia kwa msingi wa makundi matatu ya watu:

1. Wadau: watu au makundi ambayo wana ari ya kubadilika.
2. Wafanya maamuzi: watu muhimu ambao wataleta mabadiliko unayoyataka
3. Washawishi: watu wenye uwezo wa kuwashawishi wafanya maamuzi; hawa wanaweza kukuunga mkono au kukukwamisha

Matokeo maalumu ya hatua ya 3 ni makubaliano ya maofisa husika wa wilaya kushirikisha taarifa muhimu za fedha. Kama ilivyojadiliwa hapo juu (sehemu ya 3) kwa kufanya hivi wanatekeleza maelekezo mbalimbali ya serikali, lakini pia kama ipo haja, REPOA wanaweza kukusaidia katika kufanikisha azma hii.

HATUA YA 4: Itisha mkutano wa utambulisho

Hii huhitaji kufanywa katika kipindi cha siku 3, na ni vema ijumuishe taarifa nyingi zilizomo kwenye mwongozo huu, na pia itoe muda wa kujenga uelewa wa masuala ya bajeti ya wilaya kama ilivyoorodheshwa na kutumia baadhi ya taarifa muhimu za kifedha. Katika suala hili pia REPOA iko tayari kutoa ushirikiano.

HATUA YA 5: Kazi Uwandani

Madhumuni ya hatua hii ni kuunganisha ngazi za kata/kijiji, na kujenga uwezo wa makundi mbalimbali ili washiriki katika kazi za PETS kwa kufuatilia vipaumbele vyao wenyewe. Timu za kusimamia huundwa katika makundi mbalimbali, kama ilivyofafanuliwa katika sehemu ya 7. Kazi uwandani itahitaji kiasi cha majuma manne. Hii haina maana kuwa AZISE wezeshaji itatumia muda wote kijijini kwani wanajamii watahitaji pia muda kufanya hiyo kazi. Ziara kadhaa za kwenda vijijini zitahitajika wakati wa kazi uwandani.

HATUA YA 6: Mkutano Mrejesho Ngazi ya Wilaya

Katika mkutano huu, matokeo yaliyopatikana kutokana na kazi katika ngazi ya jamii yanaripotiwa kwa wanajamii, na wadau mbalimbali wanatafakari juu ya manufaa kwa jamii yaliyotokana na zoezi hilo. Mara nyingi haya huwa ni manufaa ya PETS yaliyoelezewa hapo juu katika kifungu cha 2.3. Huenda ikawa ni vema kwa mashirika ya kiraia kuitisha mkutano kabla ya mkutano mrejesho ili kuhakikisha kuwa kuna uelewa wa pamoja wa taarifa muhimu na vipaumbele.

Mkutano huu unaweza kuwa fursa kwa maafisa wa wilaya kukubaliana kushikishana taarifa za kifedha na madiwani na mashirika ya kiraia kwa vipindi vya robo mwaka, na kuwawezesha kushiriki kwa makini zaidi katika mikutano ya halmashauri. Hii ni

ufanisi kwa upande wa washiriki mbalimbali waliotajwa katika utangulizi.

HATUA YA 7: Ufuatiliaji wa Kimpangailio na Unaoendelea

Ni muhimu kwamba mashirika ya kiraia yajihusishe na mchakato badala ya kuchukulia PETS kuwa ni mlolongo wa warsha moja baada ya nyingine. Kama serikali inatoa taarifa kwa kipindi cha robo mwaka kwa washirika wengine, ni muhimu taarifa hiyo itumike. Yafuatayo yaweza kuwa sehemu ya mchakato:

- Kupanga malengo na walengwa wa kukamilisha mahitaji na vipaumbele vya makundi mbalimbali- wanawake na wanaume, watu wenye ulemavu, watu waishio na VVU n.k.
- Kuweka viashirio muafaka kusaidia kujua kuwa mahitaji yanatimizwa.
- Kufanya hesabu muhimu zitakazoonyesha gharama za kutimiza mahitaji haya.

Taarifa za msingi za kifedha kutoka katika baraza ni lazima zipitiwe kila mara na kuwekwa katika ubao wa matangazo uliokubaliwa wenye ofisi za halmashauri za wilaya. Nakala zinaweza kuwekwa katika maeneo mengine yafaayo kama mashuleni, kwenye zahanati na kwenye ofisi za vijiji. Mikutano itafanywa na wanajamii na taarifa itatayarishwa kuelezea maana na matumizi ya PETS. Hili linaweza kufanywa kwa ushirikiano na serikali za mitaa na kwa kufanya mikutano ya hadhara.

SEHEMU YA 4: Stahili na Haki - Msingi wa Kisheria na Kifedha wa PETS

Sehemu hii inaeleza kuwa kupata taarifa kwa ajili ya PETS si suala la upendeleo kutoka kwa maafisa wa serikali. Wananchi wana haki na wajibu kikatiba kupata taarifa. Zaidi ya hayo, miongozo na taratibu mbalimbali zilizotolewa na wakala (MDA) zinaipa nguvu zaidi hiyo haki. Kama maafisa wa taasisi za kijamii na serikali za mitaa watazielewa kwa ukamilifu haki na taratibu, kuanzisha PETS itakuwa ni rahisi zaidi.

4.1 Haki

4.1.1 Tunamaanisha nini kwa neno "Haki"?

Maranyingi tunasikia, tunasoma na tunaongea kuhusu haki, lakini kwa hakika tuna maana gani? Ni lazima kuwa na uelewa wa pamoja wa haki ili isaidie majadiliano yetu kuhusu haki. Tafsiri yetu ya neno haki ipo katika kisanduku 1.

Kisanduku 2: Maana ya Haki

Kwa ujumla, haki ni stahili ya kupata kitu fulani. Kwa hiyo mtu ana haki pale ambapo anastahili kutenda kwa namna fulani, au anastahili kutendewa na wengine kwa namna fulani. Kwa mfano, ukisema una haki ya kwenda nyumbani, unamaanisha kwamba unastahili kwenda nyumbani kwako (kitendo) na kwamba watu wengine wasikuzuie kwenda nyumbani.

Haki zinaweza kuwa binafsi na za ujumla. Kwa mfano, mfanyakazi mmoja peke yake, au wafanyakazi kwa pamoja katika chama cha wafanyakazi, wana haki ya uhuru wa kutofukuzwa kazi bila sababu za msingi, na haki hii inatambulika kisheria. Vilevile jamii zina haki za pamoja, kama vile za ardhi.

4.1.2 Chanzo cha Haki: Zinatoka wapi?

Kama ambavyo wakati mwingine tunaongelea haki bila kuwa na uelewa mzuri wa tunachomaanisha, watu wengi kamwe hawajui asili ya haki wanazozidai. Kuna vyanzo viwili vya haki:

- Sheria za nchi
- Kanuni na viwango vya kimaadili

Vyanzo hivi viwili vinatoa mihimili muhimu kwa haki nyingine zote ambazo mtu anaweza kudai au kuongelea. Tutazijadili zote.

Haki huweza pia kuambatanishwa katika sera fulani za serikali. Kwa mfano, Sera ya Elimu na Mafunzo (1995) inasema "Serikali itahakikisha upatikanaji wa elimu ya awali, elimu ya msingi na kisomo cha watu wazima kwa raia wote kama haki yao ya msingi" (aya ya 3.2.1, ukurasa wa 18). MKUKUTA inakazia ahadi za kisera kama hizi zenye malengo kama "mgawanyo sawa mali za umma na ushughulikiaji wa dhati wa rushwa" (Kifungu cha 3, Lengo la 2).

1. Sheria

Haki zinapokuwa na msingi wa kisheria huitwa haki za kisheria. Hizi ni haki zinazotokana na sheria zinazomruhusu au zinazompa uwezo mtu kutenda kwa namna fulani au zinazowataka watu wengine kumtendea mtu fulani kwa namna fulani. Haki za kisheria zinajumuisha haki zilizoundwa na sheria mama ya nchi, kwa maneno mengine Katiba, kwa kuwa Katiba ya nchi ndiyo msingi wa sheria nyingine zote za nchi husika.

Zifuatazo ni dondoo nyingine zinazosaidia kueleza kuhusu haki za kisheria:

- Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inawahakikishia raia wake wote waliofikia umri wa miaka 18 haki ya kupiga kura katika uchaguzi wowote wa umma utakaofanyika Tanzania. Hii ina maana kwamba mtu yeyote mwenye umri wa miaka 18 au zaidi anayo haki hii.

- Kuna haki nyingine nyingi zitokanazo na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Tazama JMT, 1998). Hizi zinajumuisha zile zilizotajwa katika Sehemu ya III ya Katiba ya Tanzania (uk. 20-33)[3].

- Kwa kuwa haki za kisheria zinatokana na mfumo wa sheria wa nchi, zinakuwa na tabia ya kuwa na nguvu ndani tu ya sheria husika ambayo kwayo mfumo huo wa sheria hufanya kazi. Kwa mfano, ingawaje Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaeleza kwamba kazi ni haki ya kila mtu, Katiba ya Marekani Kaskazini haitoi haki hii.

    - Sheria inapobainishwa katika sheria maalum, inaweza kuhuishwa mahakamani. Kwa maneno mengine, mtu anaweza kushitaki au kushitakiwa kwa ukiukaji wa haki hiyo.

    - Kubainisha haki katika nyaraka za kisheria za taifa haimaanishi kuwa sheria hiyo inazingatiwa. Kwa mfano, katiba inaweza kutoa haki ya elimu bila malipo (yaani elimu ya bure), lakini kama fedha za kugharamia hazipo haki hiyo haitatekelezwa[4].

2. Kanuni na Vipimo vya Maadili

Baadhi ya vipimo vya maadili na utu vina nguvu zaidi na ni muhimu zaidi kuliko sheria. Kwa hiyo hata kama havitajwi katika katiba au sheria za nchi husika, bado vina umuhimu. Vipimo hivi vinaundwa kwa misingi ya kimaadili na kanuni zinazobainisha kwamba binadamu wote wanaruhusiwa na wanawezeshwa kufanya kitu fulani, au wanastahili kufanyiwa jambo fulani. Hizi hufahamika kama **Haki za Kimaadili au za Kibinadamu**. Nyingi zinatajwa katika nyaraka muhimu, ambazo hufahamika kimataifa na zimeridhiwa na serikali mbambali za kitaifa. Haki hizi zinajumuisha:

- **Taarifa ya Ulimwengu ya Haki za Binadamu (1948)**

Hili ni kabrasha la msingi linalotangaza viwango na taratibu za haki za binadamu. Tangazo hili linasisitiza kutobagulika kwa haki za watu wote kama msingi wa haki sawa na amani duniani.

- **Azimio la Kuondoa Aina Zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake (CEDAW)**

CEDAW inawakilisha hati ya kimataifa yenye mchanganuo mpana zaidi na yenye nguvu za kisheria inayokataza ubaguzi wa wanawake na kuzipa wajibu serikali

kuchukua hatua rekebishi za makusudi kuleta usawa wa kijinsia.

- **Tamko la Haki za Watoto (CRC)**

Tamko hili limeridhiwa na takribani nchi zote duniani. Limekuwa ni kama tamko la dunia. CRC inatambua umuhimu wa kulinda na kuendeleza haki za watoto, kusaidia ukuaji wao ili waendelee na kuwa raia wa dunia wenye thamani bila kujali jinsia, rangi, dini wala mbari zao.

Majadiliano na Tafakari:

Kuna haki nyingi ambazo watu kwa kawaida hudai kuwa nazo. Jadili baadhi ya haki hizi utoe uhalali wake.

- Je, haki zina uhusiano wowote na maadili ya kijamii? Kuna uhalali gani wa kuziita baadhi ya haki 'za ulimwengu'?
- Kwa kuzingatia mjadala huu, elezea kama unanufaika na haki zote ulizozibainisha: zipi ni ndiyo, na zipi hapana? Kama huzifaidi, zipi zinaweza kuwa sababu za kukufanya usizifaidi?
- Je makundi mbalimbali ya watu yana uwezo tofauti katika kupata haki zao? Toa mifano na jaribu kueleza kwanini hali iko hivyo.

Haki nyingi watu wachache hawakubaliani nazo, kama haki ya kutofungwa gerezani bila kushitakiwa. Haki nyingine zinaruhusu zaidi majadiliano. Una haki ya kufanya kazi kwa kuwa tu wewe ni binadamu?

4.2 Haki, Uwazi na Upatikanaji wa Taarifa

Maana ya Uwazi

Uwazi maana yake ni upatikanaji rahisi wa taarifa zinazohitajika, kwa muda sahihi na za kuaminika kuhusu hali ya kiutendaji ya mara kwa mara, hali ya kifedha na kiutawala.

Ni sahihi kutarajia uwazi katika masuala ya kifedha ili kudumisha au kuboresha mahusiano baina ya wananchi na serikali. Wananchi katika nchi ya kidemokrasia huchagua viongozi ambao hatimaye huunda serikali. Kwa msingi kuna uhusiano kama wa tajiri na wakala wake, na katika mahusiano haya wananchi ndiyo tajiri na serikali (wizara zote, idara na kadhalika) ndiyo mawakala.

Katika mahusiano ya tajiri na wakala, wakala anawajibu wa kutoa taarifa juu ya utendaji wake, ili tajiri aamue kama utendaji wa wakala ni mzuri au mbaya. Katika suala hili serikali inatakiwa kutoa taarifa kwa wananchi ili watathmini utendaji wa serikali. Huu ndiyo msingi wa "haki ya kupata taarifa". Kwa njia ya haki ya kupata taarifa, na kwa hiyo uwazi, serikali na wakala zake mbalimbali inaweza kuwajibika kwa wananchi, kwa sababu kwa kuwa na taarifa wananchi wanaweza kuamua kuhusu utendaji wa serikali. Kwa kiasi fulani makundi yaliyosahaulika yanahitaji taarifa hizo zaidi kuliko makundi mengine kwa sababu ya shida au ugumu unaowasibu katika kupata haki zao. Hata hivyo kwa bahati mbaya hakuna sheria rasmi ya "Haki ya Kupata Taarifa" Tanzania.

4.3 Haki ya Taarifa za Fedha: Msingi wa Uwazi katika Tawala za Mitaa

Haki ya kupata taarifa si kitu kipya kwa mamlaka za ndani. Kuna nyaraka mbalimbali za kisheria na kisera zinazounda mfumo wa uwazi Tanzania. Hizi ni pamoja na:

- Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,
- Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya 1982,
- Miongozo ya Mipango na Bajeti itolewayo kila mara na OWM-TAMISEMI kwa ajili ya matumizi ya serikali za mitaa. Tambua kwamba Mpango wa Muda wa Kati wa OWM-TAMISEMI 2005-2008 unasisitiza kiwango cha juu cha uwazi hasa katika masuala ya fedha.
- Kiongozi cha makadirio cha TAMISEMI.

Kila kimoja kitachanganuliwa baadaye.

4.3.1 Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania

Katiba ya Jamhuri ya Muungano waTanzania inaeleza wazi kwamba wananchi wana haki ya kupata taarifa. Kifungu cha 18 kinaeleza kwamba:

(1) …. kila mtu ana haki ya kutoa mawazo na kujieleza, kutafuta, kupokea na kutoa taarifa na mawazo kwa njia yoyote ndani na nje ya mipaka ya nchi, na pia ana haki ya kutoingiliwa katika mawasiliano yake.

(2) Kila mwananchi ana haki ya kupata taarifa kuhusu matukio mbalimbali ya kitaifa au ya kidunia wakati wote ambayo yana umuhimu kwa maisha na shughuli za watu na masuala muhimu kwa jamii.

Kwahiyo, haki ya taarifa, ikijumuisha haki ya kupata taarifa za kifedha, inaundwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

4.3.2 Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa Na. 9 ya 1982 na Taarifa ya Fedha ya Serikali za Mitaa, 1997

Sheria ya utekelezaji wa taarifa za fedha ni Sheria Na. 9 ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya 1982. Sheria hii hubainisha kwa uwazi aina ya taarifa za fedha zinazotakiwa kuwekwa wazi.

Taarifa ya Fedha ya Serikali za Mitaa, 1997 inafafanua maana ya sheria hii kiutendaji. Kwa mfano:

- Inatoa maelezo ya kina juu ya majukumu ya maafisa mbalimbali wa Wilaya na vyombo mbalimbali vya Wilaya, ikwa ni pamoja halmashauri yote kuhusiana na usimamizi wa fedha katika halmashauri. Maafisa hawa ni pamoja na Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya (DED), Mhazini wa Wilaya (DT) na Mdhibiti Mahesabu wa Ndani (IA) n.k.
- Pia inatoa njia ambazo kwazo ripoti za kifedha zilizoandaliwa na Halmashauri zitapatikana, kama kwa njia za machapisho ya taarifa za fedha katika magazeti, matangazo kwenye mbao za matangazo na kwingineko.

4.3.3 Miongozo ya Mipango na Bajeti ya OWM-TAMISEMI

Mpango wa Muda wa Kati na Miongozo ya Kuandaa Mipango na Bajeti ya 2005-2008 zilitolewa na OWM-TAMISEMI kwa Serikali za Mitaa. Zinasistiza Serikali za Mitaa ziwe wazi katika mchakato wa kupanga na kubajeti, kwa kushirikishana mipango na bajeti na wadau mbalimbali, ikiwa ni pamoja na asasi za kijamii.

Mpango wa Muda wa Kati wa LGRP wa 2005-08, unasema kwamba asasi za kiraia zina nafasi bora zaidi kutekeleza PETS katika jamii zao. Unaeleza kwamba:

Upande wa mahitaji wa mlinganyo wa taarifa ndipo hasa ASIZE zina nafasi kuwa zaidi. OWM-TAMISEMI wataomba ushauri na mawazo jinsi gani watumiaji wa huduma wanaweza kutumia taarifa kupanga mambo muhimu na kuishawishi Serikali, (JMT, 2005).

Pia miongozo ya bajeti ya OWM-TAMISEMI ya 2006/07-2008/09 inatoa maelekezo maalumu juu ya masuala ya jinsia, kama ifuatavyo:

> Aya ya 36: Jinsia: Mamlaka ya Serikali za Mitaa imewateua wataalamu watakaoshughulikia masuala ya jinsia katika ofisi zao. Maelekezo ya kuainisha masuala ya jinsia katika mchakato wa Mipango na Bajeti yanaandaliwa.
>
> Aya ya 51: Masuala ya jinsia yanayogusa pande zaidi ya moja: Serikali itaendelea kupunguza msigano wa muda mrefu baina ya wanaume na wanawake kwa njia ya utekelezaji wa Sera na Mikakati ya Jinsi.
>
> Serikali za Mitaa na Halmashauri za Wilaya zinatakiwa kujumuisha masuala ya kijinsia katika sera na mikakati ya mabaraza katika ngazi zote na kuboresha uwezo wa kuratibu vipengele vya jinsia na kuhamasisha jamii juu ya fursa sawa na usawa wa jinsia.

4.3.4 Mwongozo wa Kipimo cha PMSM

Programu ya Maboresho ya Serikali za Mitaa (PMSM) imejumuisha uwazi katika masuala ya fedha katika mwongozo wake wa kipimo kama kigezo kimojawapo cha kupimia Serikali za Mitaa kila mwaka kama njia ya kupima utendaji. Mambo mengine ni pamoja na:

- Kiasi walichofanikiwa baada ya kupata msaada.
- Kama taarifa hutolewa kwenye mbao za matangazo.

Hii inaendana na matakwa ya miongozo ya mipango na bajeti juu ya uwazi. Tathmini hizi za kila mwaka ni ishara nzuri ya uwazi katika ngazi ya jamii.

4.3.5 Msaada wa Maendeleo ya Majengo wa Serikali za Mitaa (LGCDG)

Vigezo vya LGCDG pia hukuza uwazi kwa masharti yao katika utoaji wa misaada. Nakala nzima ya vigezo au masharti haya inapatiaka REPOA, lakini inajumuisha mambo yafuatayo kama hatua za kutahmini utendaji:

- Ushahidi kwamba taratibu za mipango shirikishi zimefuatwa kwa kuzingatia miongozo ya mipango kwa njia ya kumbukumbu za kikao cha Kamati ya Baraza la Uongozi kuonyesha kama kweli wameingiza mipango ya maendeleo kuanzia ngazi za chini za uongozi.
- Kama mchakato wa mipango unaonyesha ushahidi wa ushiriki wa wadau

wengine ambao utaonyeshwa kenye kumbukumbu za kazi za afisa mipango.

- Kuonyesha kama mambo ya jinsia na mazingira yamezingatiwa katika mipango.
- Kwamba taarifa mpya za fedha zinawekwa katika mbao za wazi za matangazo katika makao makuu ya serikali za mitaa na katika maeneo mengine ya wazi.
- Miradi iliyopitishwa ya mwaka katika maeneo mbalimbali ya serikali za mitaa inawekwa wazi katika ofisi husika za serikali na katika maeneo mengine ya wazi.

4.3.5 MKUKUTA

Vifungu vya Utawala na Uwajibikaji vina umuhimu wa pekee hapa. Lengo la pili linahusu mgawanyo sawa wa mali za umma, huku rushwa ikiwa imedhibitiwa ipasavyo. Mikakati ifuatayo ya kifungu hicho ni muhimu:

2.1.1 Kuhakikisha kuwa Mapitio yote ya Matumizi ya Umma (PER) yanazingatia masuala ya mgawanyo sawa na usawa wa jinsia katika ufuatiliaji wa matumizi ili kusimamia matumizi ya bajeti inayowajali wenye kipato kidogo, kwa kuzingatia mahitaji ya watu maskini na makundi yaliyosahauliwa kijamii.

2.1.3 Kuongeza ushiriki wa kina wa umma katika kuandaa, kuunda na kusimamia Mkakati wa Kupunguza Umaskini, Mapitio ya Matumizi ya Umma (PER) na bajeti, ikijumuisha utoaji taarifa hadi ngazi za chini kabisa za jamii kuhusu bajeti, matumizi na mapato.

2.1.6 Kuongeza uelewa wa watu kuhusu sera za serikali, fedha za umma na gharama za maafisa pamoja na stahili zao kwa njia ya elimu ya uraia na kwa kusambaza taarifa.

2.1.9 Kuimarisha mifumo na taasisi za uwajibikaji, maadili, uwazi serikalini, na wa maafisa wasio serikalini pamoja na vyama vya siasa.

Majadiliano na Tafakari:

"Umma" uanoongelewa katika vifungu hivi vya mikakati ni akina nani ? Je, baadhi ya makundi yana ufahamu zaidi ya mengine? Kwa nini? Je ni rahisi kwa baadhi ya makundi kushirikishwa kuliko mengine? Kwa nini?

Kwa kifupi, suala la PETS linafahamika vizuri katika ngazi ya sera na miongozo ya utekelezaji. Changamoto ni utekelezaji wa vitendo.

SEHEMU YA 5: Mipango na Bajeti Ngazi ya Wilaya

Lengo la kipengele hiki ni kutambulisha mawazo na taarifa muhimu ambazo unahitaji kufahamu na kuizingatia unapofikiria kuanzisha PETS.

5.1 Kuelewa namna ya Kuandaa Bajeti ya Wilaya

Mchoro ufuatao unaelezea mchakato wa bajeti ya wilaya. Uelekeo huu wa uchambuzi, mipango, utekelezaji, usimamizi na tathmini unaweza pia kufuatwa katika mazingira ya aina tofauti na taasisi tofauti. Ni muhimu kulielewa hili ili ujue ni wapi kuna fursa ya kuingia kwenye mchakato wenyewe na kujaribu kufanya ushawishi.



Mzunguko huu hufuatwa kila mwaka kama unavyoonyeshwa kwenye kisanduku kifuatacho. Hii inajumuisha mchakato wa mipango na kuandaa bajeti kwa ajili ya shughuli za maendeleo ambazo zitagharamiwa kwa njia ya LGCDG. Ni muhimu kulifahamu hili ili kujua fursa zilipo za wewe kujihusisha katika mchakato na kujaribu kufanya ushawishi.

Mwezi	Tukio
Septemba	Tathmini ya utendaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa mwaka uliopita kwa ajili kuwasilisha PMO-RALG
Desemba	PMO-RALG inachapisha mgao wa Msaada wa Ujenzi na Kujenga uwezo chini ya LGSP (Indicative Planning Figures - IPF) pamoja na miongozo kwa mwaka ujao.
Desemba-Januari	Mamlaka za Serikali za Mitaa wanaandaa mipango ya awali na bajeti, na kuwataarifu Kamati za Maendeleo za Kata (WDC) na Kamati za Vijiji (VCs) juu ya miongozo na asilimia 50 ya IPF inatakiwa kugawiwa kwenye kata na vijiji.
Februari	Vijiji vinaanda mipango ya maendeleo na bajeti kwa kutumia njia ya O&OD vikisaidiwa na wawezeshaji wa kata na wilaya.
Machi	WDC inapitisha mpango Wanakijiji wafanya mkutano kupitisha mpango WDC inathibitisha mipango ya kijiji na kuiwasilisha kwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Wilaya inaandika Mpango wa mwisho wa Maendeleo wa Wilaya
Aprili	Wilaya inapitia Mpango wa Maendeleo wa Wilaya na kuupeleka Kamati ya Ushauri ya Mkoa Kamati ya Ushauri ya Mkoa inatoa mapendekezo Mamlaka ya Serikali za Mitaa inawasilisha mpango kwa baraza kuu la madiwani ili upitishwe. Baraza linaweza kukataa mapendekezo ya RAC lakini haliwezi kufuta miradi iliyopitishwa na WDC ambayo inapata fedha kutoka IPF.
Mei	Mamlaka ya Serikali za Mitaa inawasilisha mpango uliopitishwa kwa OWM-TAMISEMI na Wizara ya Fedha
Juni	Bunge linapisha Bajeti ya Taifa
Julai-Agosti	Wizara ya Fedha inatoa fedha kwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa, mamlaka pia inachapisha tangazo kuhusu mgao wa fedha zilizopitishwa kwa kata na vijiji
Agosti	Mamlaka za Serikali za Mitaa zinaanza kutekeleza mipango

5.2 Vyanzo vya Taarifa za PETS

Kuna uwezekano wa kupata taarifa kupitia vyanzo vingi kama ilivyoorodheshwa hapa chini. Ni vema kutumia chanzo zaidi ya kimoja ili kuthibitisha usahihi wa taarifa.
Kwa kufanya kazi karibu na maofisa wa wilaya unaweza kuzalisha na kusambaza taarifa juu ya mapato na matumizi. Taarifa hizi zikiwekwa wazi, kuna uwezekano wa kuboresha upangaji wa bajeti na huduma.

Chanzo cha Taarifa	Maelezo
Ripoti za Kiutawala za robo mwaka	• Hizi huandaliwa kwa kipindi cha robo mwaka na timu ya wilaya ili kuonyesha namna fedha zilivyoingia wilayani na jinsi zilivyotumika • Ripoti hizi kwa kawaida huwasilishwa katika baraza kuu la madiwani. • Mashirika ya kiraia yanaweza yanaweza kupata nakala za ripoti hizi kutoka wilayani baada ya kujadiliwa.
Matangazo ya robo mwaka ya kupokea/kutoa fedha	Kwa kawaida wilaya zinapopokea fedha kutoka serikali kuu, huzitangaza kwenye mbao za matangazo.
Nyaraka za Muundo wa Matumizi ya Fedha wa Muda wa Kati wa Wilaya	Hizi nyaraka ni muhtasari wa mipango na bajeti wa wilaya na huandaliwa kwa mwaka mara moja kwa vipindi vya miaka mitatu. Pia huwasilishwa kwenye baraza kuu la madiwani na kwenye serikali kuu OWM-TAMISEMI.
Taarifa zilizokaguliwa za fedha	• Taarifa za mapato na matumizi, mizania, na Taarifa za Uelekeo wa Kifedha pamoja na urari. • Tovuti ya Serikali ya Tanzania inayo taarifa ya Mkaguzi Mkuu.
Makadirio ya Bajeti ya Wilaya	Nyaraka hizi huhifadhiwa na Muhazini wa Wilaya
Taarifa za mwaka zitolewazo kwenye LAAC	Hizi ni nyaraka fafanuzi zaidi zinazoandaliwa wilayani na zinajumuisha kwa kina masuala yote ya kifedha.
Miongozo ya Mipango na Bajeti ya OWM -TAMISEMI kwa ajili ya Serikali za Mitaa.	Chini ya mfumo mpya wa kupeleka fedha wilayani, OWM -TAMISEMI walitoa miongozo inayoonyesha kwa kawaida wilaya au mkoa utapokea kiasi gani cha fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo na pia kama matumizi mengineyo.
Mahojiano na wajumbe wa uongozi wa wilaya	Hasa wakuu wa idara wanaweza kuwa wa msaada
Vyombo vya habari	

Kukiwepo na taarifa za kina kama hizi, ni rahisi kuelewa kwa nini kuanzishwa kwa PETS kunaungwa mkono kikamilifu na serikali za mitaa.

5.3 Taarifa za Ugavi

Taarifa za mapato na mizania zinapatikana katika kila halmashauri. Hili ni sharti la kisheria, ambalo hudhihirisha jinsi taarifa hizi zilivyo muhimu.

5.3.1 Taarifa za Mapato

Hii ni taarifa ya mapato ya Simanjiro ya mwaka 2003:

Chanzo cha Gharama	Mchanganuo wa Mapato	Makadirio yaliyoidhinishwa	Mapato halisi
	Fedha, Mipango na Utawala	206,195,900	209,412,110
	Afya	249,690,870	189,086,699
	Elimu	611,090,060	562,984,805
	Kilimo	54,782,500	50,495,900
	Mageuzi ya Serikali za Mitaa	172,314,000	34,427,880
	Mishahara	605,800,200	601,663,242
	Maalum	16,406,600	15,838,100
	Maji	78,844,100	108,768,600
	Maendeleo	70,000,000	68,750,000
	Mfuko wa Barabara	127,400,000	124,601,917
	Jumla ya Mapato	2,192,524,230	1,966,029,253
Upungufu katika Matumizi:			
Maelezo ya Matumizi		Makadirio yaliyoidhinishwa	Matumizi halisi
	Fedha, Mipango& Utawala	206,195,600	220,971,024
	Afya	249,690,870	228,504,162
	Elimu	611,090,060	596,077,150
	Kilimo	54,782,500	71,511,978
	Mageuzi ya Serikali za Mitaa	172,314,000	33,392,760
	Mishahara	605,800,200	574,242,220
	Maalum	16,406,600	17,067,546
	Maji	78,844,100	58,089,891
	Maendeleo	70,000,000	44,913,744
	Mfuko wa Barabara	127,400,000	148,902,801
	Polisi	15,000,000	2,478,150
	Jumla ya Matumizi	2,207,523,930	1,996,151,426
	Ziada/Upungufu kwa mwaka 2003 Tshs.	0	- 30,122,173
	Ongeza: Ziada/Upungufu b/f Tshs.	0	998721143
	Ziada Limbikizi	0	968,598,970

Majadiliano na Tafakari:

Unapata ujumbe gani kutokana na taarifa hii? Taarifa hii ina manufaa gani katika uwajibikaji? Kuna chohote unachoweza kubadilisha katika namna ambavyo taarifa hii imetolewa?

5.3.2 Mizania

Majadiliano na Tafakari:

Unapata ujumbe gani kutokana na mizania hii? Ina manufaa gani katika uwajibikaji? Kuna chohote unachoweza kubadilisha katika namna ambavyo taarifa hii imetolewa?

Kama msingi wa warsha ya kwanza iliyoelezewa katika hatua ya 4 hapo juu, lengo kukusanya taarifa muhimu zitakazowesha kujaza kisanduku kifuatacho kwa usahihi kadri iwezekanavyo.

Jedwali la 3: Mfano wa Muundo wa Fomu ya PETS

SEKTA	**Iliyobajetiwa**	**Zilizopokelewa**	**Zlizotumika Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya**	**Zilizopelekwa/ Zilizotumika vijijini**		**Baki**
				Zilizotumika	Zilizotumika	
ELIMU						
AFYA						
KILIMO n.k.						
Jumla						

Nakala kamili ya fomu hii imeambatishwa kama kiambatisho cha pili. Inaweza kutumika na baadhi ya sekta, au mkazo unaweza kuwa katika kuhamisha fedha kwenye kijiji au makundi ya vijiji, badala ya ngazi ya kijiji kwa ujumla.
Unapojaribu kupata taarifa kwa ajili ya kujaza fomu hii, kumbuka kwamba kuna vyanzo vingi vya fedha za serikali ya wilaya. Hii humaanisha pia kwamba kuna taarifa nyingi za fedha zinazotakiwa kupatikana hata katika hatua za chanzo kimoja kimoja.
Taarifa zinaweza kutengwa kwa visanduku vya sekta kwa sekta, au zikaanikwa kwenye kisanduku kimoja kikubwa, kama kwenye kipengele cha 4.7.1.

5.4 Mifano Mitatu ya Matokeo ya PETS

5.4.1 Matokeo yanayojumuisha Halmashauri yote ya Wilaya

Jedwali lifuatalo lifuatalo linaonyesha matokeo ya PETS moja katika Halmashauri ya Wilaya ya Singida ya Aprili 2006. jedwali bado halijakamilika. Hata hivyo, taarifa yotote itakayopatikana itakuwa ni hatua kubwa ukilinganisha na mfumo uliopo, na inaweza kushindikana kujaza taarifa zote katika fomu hii. Kama baadhi ya taarifa haziwezi kupatikana, safu zisizojazwa bado zionyeshwe kama kumbukumbu kwamba baadhi ya taarifa hazijakamilika.

PETS kwa Mwaka 2004/05

SEKTA	Zilizobajetiwa	Zilizopokelewa	Zilizotumiwa na Halmashauri ya Wilaya	Zilizopelekwa Vijijini	Baki
ELIMU					
Matumizi Mengine	459,410,000	459,413,000	190,988,040.77	268,040,974	383,985.23
Ruzuku kwa kila mtu	0	326,360,612	0	326,360,612	0
Msaada wa Maendeleo	0	687,399,005	0	687,399,005	0
Msaada wa Kujenga Uwezo	0	0	0	0	0
	0	0	0	0	0
	0	0	0	0	0
Mapato ya Vyanzo Ndani ya Halmashauri	0	0	0	0	0
Jumla	459,410,000	1,473,172,617	190,988,040.77	1,281,800,591	383,985.23
AFYA					
Matumizi Mengine	269,204,900	321,143,200	320,086,288.70	0	1,056,911.3
Maendeleo	0	0	0	0	0
Ruzuku ya CHF	0	0	0	0	0
	0	0	0	0	0
	0	0	0	0	0
Mapato ya Halmashauri	0	0	0	0	0
Jumla	269,204,900	321,143,200	320,086,289	0	1,056,911
BARABARA					
Mfuko wa Barabara	175,071,500	154,169,640	0	153,684,535.80	485,104.2
Mapato ya Halmashauri	0	0	0	0	0
Jumla	175,071,500	154,169,640	0	153,684,536	485,104
KILIMO					
Matumizi Mengine	42,318,600	40,183,600	39,184,200	0	999,400
DADP	77,185,584	77,185,584	0	77,185,584	0
PADEP	227,659,150	227,659,150	0	227,659,150	0
Mapato ya Halmashauri	17,500,000	5,153,900	5,053,900	100,000	0
Jumla	364,663,334	350,182,234	44,238,100	304,944,734	999,400
UJENZI					
Matumizi Mengine	18,700,000	18,699,000	18591861.95	0	107,138
Maendeleo	0	0	0	0	0
Mapato ya Halmashauri	0	0	0	0	0
Jumla	18,700,000	18,699,000	18,591,862	0	107,138
MAJI					
Matumizi Mengine	72,674,300	68,229,100	66,867,165.23	0	1,361,934.77
Maendeleo.	0	0	0	0	0
Mapato ya Halmashauri	0	35,218,270	0	0	0
Jumla	72,674,300	103,447,370	66,867,165	0	1,361,935
BAJETI HURIA					
LGCDG	0	0	0	0	0
LGDG	0	0	0	0	0
	0	0	0	0	0
	0	0	0	0	0
Mapato ya Halmashauri	0	0	0	0	0
Jumla	0	0	0	0	0
Jumla Kuu	1,359,724,034	2,420,814,061	640,771,457	1,740,429,861	4,394,474

Chanzo cha Taarifa: Vitabu vya Hesabu na rekodi nyingine zilizohifadhiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Singida

Ufuatiliaji wa Matumizi ya fedha za Serikali kwa nusu mwaka wa 2005/06

SEKTA	Zilizobajetiwa	Zilizopokelewa	Zilizotumiwa Halmashauri ya Wilaya	Zilizopelekwa vijijini	Salio
ELIMU					
Matumizi Mengine	477,445,050	484,830,200	471,822,899.91	0	13,007,300
Ruzuku kwa kila mtu	0	13,103,029	0	13,103,029	0
Msaada wa Maendeleo	0	0	0	0	0
Msaada wa Kujenga Uwezo	0	0	0	0	0
Mapato ya ndani ya Halmashauri	0	0	0	0	0
Jumla	477,445,050	497,933,229	471,822,899.91	13,103,029	13,007,300
AFYA					
Matumizi Mengine	195,095,850	203,200,600	148,104,475.71	0	55,096,124.3
Maendeleo	0	0	0	0	0
Ruzuku ya CHF	0	0	0	0	0
Mapato ya ndani ya Halmashauri	0	0	0	0	0
Jumla	195,095,850	203,200,600	148,104,476	0	55,096,124
BARABARA					
Mfuko wa Barabara	127,903,900	66,492,472	0	51,136,808.00	15,355,664.1
Mapato ya ndani ya Halmashauri	0	0	0	0	0
Jumla	127,903,900	66,492,472	0	51,136,808	15,355,664
KILIMO					
Matumizi Mengine	40,144,000	26,033,500	20,014,671	0	6,018,829
DADP	0	52,121,000	0	52,121,000	0
PADEP	0	383,974,670	0	383,974,670	0
Mapato ya Halmashauri	5,450,000	0	0	10,000,000	0
Jumla	45,594,000	462,129,170	20,014,671	446,095,670	6,018,829
UJENZI					
Matumizi Mengine	13,084,050	12,005,500	4035664.44	0	7,969,836
Maendeleo	0	0	0	0	0
Mapato ya ndani ya Halmashauri	0	0	0	0	0
Jumla	13,084,050	12,005,500	4,035,664	0	7,969,836
MAJI					
Matumizi Mengine	34,656,150	37,023,300	25,874,550.72	0	11,148,749.28
Maendeleo	0	0	0	0	0
RWSSP	0	150,000,000		150,000,000	
Mapato ya Halmashauri	33000000	15,000,000	0	15,000,000	0
Jumla	67,656,150	52,023,300	25,874,551	150,000,000	11,148,749
BAJETI HURIA					
LGCDG	0	0	0	0	0
LGDG	0	0	0	0	0
Mfuko wa Jumla	438,818,700	225,704,773	225,704,773	0	0
	0	0	0	0	0
LAMP	267500000	146865000	20518700	126,346,300	0
Mapato ya Halmashauri	0	0	0	0	0
Jumla	706318700	372569773	246223473	126346300	0
Jumla Kuu	1,633,097,700	1,666,354,044	916,075,735	786,681,807	108,596,502

Chanzo cha Taarifa: Vitabu vya hesabu na kumbukumbu nyingine zilizohifadhiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Singida **(Taarifa zilikusanywa Aprili, 2006)**

5.4.2 Matokeo kwa Sekta Moja

Jedwali lifuatalo linatoa muhtasari wa zoezi la PETS lililofanywa wilayani Babati mwezi Januari 2006. Zoezi lilihusisha sekta ya kilimo pekee, lakini linatoa habari muhimu. Kisanduku cha 1 ni juu ya upatikanaji wa fedha katika sekta ya kilimo kwa mwaka wa fedha wa 2004/05. Picha ya jumla inayojitokeza ni kwamba fedha nyingi zilizopatikana zilitumika makao makuu ya wilaya. Kwa mfano, wilaya ilipokea shilingi milioni 539/= kutoka vyanzo mbalimbali katika mwaka husika, shilingi milioni 356.5/= makao makuu ya wilaya na kiasi cha shilingi milioni 151/= zilitumika katika ngazi ya kijiji. Pia kwa ujumla, wilaya ilipokea fedha pungufu kuliko zile ambazo ilikadiria kwenye bajeti. Kiasi cha upungufu kilikuwa shilingi milioni 74.5/=.

Jedwali 1. Uelekeo wa Kifedha wa Halmashauri ya Wilaya ya Babati kwa Mwaka 2004/05 Sekta ya Kilimo (Viwango katika TSh.)

Kifungu cha Bajeti	Bajeti	Zilizopokelewa/ kusanywa	Zilizotumika Makao Makuu ya Wilaya	Zilizotumika ngazi ya kijiji	Baki
Kilimo na Mifugo					
Kutoka Serikali Kuu: Matumizi Mengine (OC)	21,476,100	34,017,039	27,969,660	3,851,800	2,195,579
Fedha za Maendeleo (uwekezaji)					
DADP (kutoka srikali Kuu-MAFS)	30,396,248	30,396,248	0	30,396,248	0
PADEP	0	115,705,500	86,884,215	26,962,500	1,858,785
LAMP	79,691,800	79,691,800	0	53,425,840	26,265,960
Jumla					

Chanzo: Kumbukumbu za wilaya

Jedwali 2: Mapato ya Halmashauri

Matumizi	Bajeti	Kiasi cha fedha kilichokusanywa /kupokelewa	Kilichotumika Makao Makuu ya Wilaya	Kilichotumwa/ kutumiwa ngazi ya kijiji	Baki
Matumizi Mengine	456,890,154	245,184,409	208,893,646	36,290,763	0
Kusaidia Vyama vya Ushirika/SACCOS	9,457,800	1,297,150	1,297,150	0	0
Mchango wa Wilaya kwenye shughuli za LAMP	15,745,000	15,745,000	15,745,000	0	0

Chanzo: Kumbukumbu za Wilaya

Kufuatana na viwango vilivyokuwa vimetengwa kwenye matumizi mengine (OC) Kilimo na Mifugo zilitumia fedha zaidi ya kiasi kilichokuwa kimetarajiwa. Kiasi kikubwa cha fedha iliyopokelewa (asilimia 82) kilitumiwa ngazi ya wilaya (tazama Jedwali 2). Hii humaanisha kwamba maafisa wa kilimo walio vijijini wanaweza kuwa hawakupata fedha ya kutosha kutoa ushauri wa kitaalam. Matokeo yake ni huduma duni za kilimo vijijini.

Hoja za Majadiliano:

- Je, wawezaje kukadiria kiwango ambacho wanawake na wanaume hunufaika na bajeti hii?
- Je, bajeti hutusaidia kujua kiasi cha msaada kwa ajili ya uzalishaji wa mazao ya chakula ikilinganishwa na mazao ya biashara? Tafadhali elezea.
- Je, kuna faida na mapungufu yapi katika utoaji wa taarifa wa namna hii?
- Je, unaona mianya ya mafanikio na vikwazo gani dhidi ya shughuli ya namna hii? Vikwazo hivi vinaweza kudhibitiwa namna gani?

5.4.2: Matokeo kutokana na Mtazamo wa Kijinsia

Matokeo yanaweza kuchambuliwa kutokana na mtazamo wa kundi lililotengwa kijamii. Mfano ufuatao umefikiwa kwa kutumia mtazamo wa kijinsia, lakini kanuni zile zile zaweza kutumiwa na kundi jingine lolote lililotengwa.

Kipengele B
Mitazamo ya Kukamilishana katika Utekelezaji wa PETS

Utangulizi

Kufuatia mitazamo iliyokwishaelezwa juu ya utekelezaji wa PETS, ni wazi kwamba kiwango cha msisitizo tu ndicho chaweza kuonyesha utofauti, hasa kuendana na mahitaji ya mtumiaji wa PETS.

Mbali na kwamba mitazamo imefafanuliwa tofauti tofauti, inaweza kuunganishwa na kufanya kazi kwa mafanikio. Zana za muundo mmoja zaweza kutumiwa kuboresha muundo mwingine. Hakuna njia inayoweza kusemwa kuwa bora kuliko zote, bali yategemea tu kipengele unacholenga kusisitiza (kufuatilia kwa karibu) katika PETS. Na kadiri unavyoendelea kujishughulisha na masuala ya PETS na kuwa mzoefu, waweza kupanua ufuatiliaji wako na kushughulikia mambo mengi zaidi.

MTAZAMO WA KWANZA: Kusisitiza mahitaji ya makundi yaliyotengwa na jamii 'kusisitiza masuala ya kijinsia'

MTAZAMO WA PILI: Kusisitiza kuijengea jamii uwezo

SEHEMU YA 6: MTAZAMO WA KWANZA: Kufanya PETS ihudumie makundi yaliyotengwa na jamii

Kwa jinsi ulivyofafanuliwa hapa, mtazamo huu unasisitiza masuala ya jinsia, lakini kanuni hizi hizi zaweza kutumiwa kwa mafanikio na makundi mengine yaliyosahaulika kama vile jamii za kichungaji, watoto wa mitaani na kadhalika.

6.1 Hatua ya Kwanza: Kuhakikisha kwamba dhana za msingi zinaeleweka

Huu mtazamo haulengi tu kupata taarifa juu ya mapato na matumizi. Unalenga pia kuelewa masuala ya jinsia na makundi ya jamii jinsi yanavyotazamwa na kushughulikiwa katika sera za uchumi, mipango, bajeti na menejimenti. Kwa hiyo ni muhimu kuanza kwa kuhakikisha kwamba mchango au athari za sera kwenye masuala ya jinsia na umasikini zinaeleweka vema.

Mawazo ya msingi ni pamoja na:

1. Kutengeneza Bajeti kwa Kuzingatia Masuala ya Jinsia

Hii humaanisha kuichambua bajeti kwa mtazamo makini zaidi wa kijinsia ili kuhakikisha kwamba usawa wa jinsia umezingatiwa katika mchakato mzima wa uandaaji wa bajeti. Hii haimaanishi kuifanya iwe 'bajeti ya wanawake', bali kuichambua kwa makini bajeti kwa kuzingatia jinsi inavyogusa makundi tofatuti ya wanawake na wanaume. Kitu cha msingi zaidi ni kujenga 'uchumi unaojali', yaani kuangalia jinsi ya kuendeleza na kulinda wanajamii kama vile watoto, wagonjwa na wazee.

Bajeti ya kijinsia inasisitiza kuweka kipaumbele katika ugawaji wa fedha ili kuwezesha kuwepo na usawa wa jinsia, hata kama pesa iliyopo ni kidogo. Mtazamo huu wa uandaaji wa bajeti unahitaji pia kuwepo na juhudi ngazi ya taifa, wilaya au hata kisekta. Gender budgeting inatazama mchakato mzima pamoja na uchambuzi, ambavyo kwa pamoja hutusaidia kupata maarifa juu ya msigano wa jinsia na juu

ya masuala ya fedha ya umma. Gender Budgeting yaweza kulenga bajeti nzima ya wilaya, ama ya baadhi tu ya sekta au miradi katika jamii husika.

2. Sababu za Kuandaa bajeti ya kijinsia

Kuna sababu nne za kufanya bajeti ya kijinsia

- Utendaji bora hufanikisha shughuli kulingana na matumizi. Uorodheshaji wazi wa matumizi huficha mapungufu.
- Husaidia kuleta uwajibikaji na usawa wa jinsia (Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Sera ya Taifa Juu ya Masuala ya Jinsia, CEDAW, Umoja wa Maendeleo wa Nchi za Kusini mwa Afrika [SADC], Umoja wa Afrika [AU] na Beijing)
- Husaidia kuboresha msimamo na mchango wa kifedha juu ya masuala ya usawa wa jinsia.
- Husaidia kuleta utawala bora: wanawake na wanaume kwa pamoja wanayo haki ya kupata taarifa na kushiriki katika masuala yanayowahusu.

3. Mahitaji ya kuandaa bajeti ya kijinsia

- Tumia zana na mitazamo changanuzi ya kijinsia
- Uelewa wa masuala ya kijinsia yahusuyo wanawake, pamoja na taarifa tofauti tofauti.
- Kuzichunguza sera zihusuzo mahusiano ya kijinsia
- Kutambulika wanawake na mchango wao, hasa kwa kazi za kuitunza jamii (katika hatua tofauti tofauti) ambazo kwazo hawapati kipato chochote
- Wanaume na wanawake
- Kaya masikini

4. Nyanja za Kijinsia katika Bajeti ya Wilaya

Kuna makundi matatu ya bajeti zigusazo masuala ya jinsia

1) Matumizi ya kitaalam yaliyobainishwa na wilaya kwa misingi ya jinsia:

- Miradi ya wanawake juu ya matatizo yatokanayo na utofauti wa jinsia

2) Matumizi ya wilaya katika kukuza fursa sawa miongoni mwa watumishi ngazi ya wilaya:

- Kuwapa mafunzo viongozi wa kike, viongozi wa kidini na wengineo,
- Kuendesha programu maalum za masomo kwa ajili ya wanawake,
- Kuzungumzia masuala mahsusi kwa ajili ya wanawake, kama vile kuwapa msaada juu ya huduma ya uangalizi wa watoto, kupata vifaa kuwasaidia katika utoaji wa huduma hii, elimu ya uzazi, na msaada wa jinsi ya kuwahudumia wagonjwa.

3) Madhara au athari za matumizi ya jumla (katika bajeti) juu ya suala zima la jinsia.

Sehemu inayobakia ya bajeti ya wilaya iashirie lengo la kuleta usawa wa kijinsia. Maswali ya msingi hapa yaweza kuwa:

- Ni akina nani wanapata moja kwa moja huduma za wilaya?
- Nani hupokea msaada?
- Huduma zitolewazo zina manufaa (au madhara) gani?
- Nk.

Zana ya kwanza: Mazoezi ya Vitendo kwa ajili ya Kujadili Mawazo ya Msingi juu ya Jinsia

Kujaza fomu hii na kulijadili kutasaidia kuhakikisha kwamba washiriki katika warsha wanaelewa vema kiasi kikubwa cha mawazo ya msingi.

Fomu 3: kutafakari kufuatia mahitaji halisi na majibu yaliyotolewa

Majukumu ya kawaida ya uzalishaji na majukumu ya jamii katika masuala ya jinsia	*Mahitaji ni yapi?*		*Uingilizi wa Serikali*	
	Ya kiutendaji	*Ya kimkakati*	*Serikali kuu*	*Serikali ya Mtaa*

6.2 Zana za Kuuboreshea Mtazamo wa Kwanza

Nyenzo zifuatazo zaweza kutumika kusaidia katika hatua tofauti za mtazamo huu. Baadhi ya nyenzo za mtazamo wa pili zaweza pia kutumika hapa.

Nyenzo ya kwanza: Tathmini (isiyohusisha jinsia) ya vipaumbele vya wananchi katika bajeti na huduma

Taarifa za kujaza (kwenye fomu namba 4 hapa chini) zaweza kupatikana kwa kukusanya maoni ya watu, tafiti juu ya mitazamo ya watu, michakato shirikishi ya kutathmini ikiwamo makundi ya mijadala, uchunguzi shiriki, usaili nk.

- Kukusanya maoni na mitazamo ni njia za kitakwimu zaidi, zinashughulika na mtu mmoja mmoja, na maoni yapatikanayo kwa njia hii hayatokani na majadiliano na tafakuri. Kwa hiyo maoni haya yaweza kuwa hayana upeo wa kutosha, ya kupita tu na yasiyo na ulinganifu.
- Michakato shirikishi ya kutathmini (yaani Participatory rapid appraisal processes) ni njia stahilivu na ya kina zaidi ya kuyatazama maoni, ambayo hufanyika kwa kufanya upembuzi wa pamoja wa maoni na majadiliano juu ya mada ili kuwezesha watu kujifunza. Maoni haya yanatokana na majadiliano na tafakuri lakini hayawezi kuonyeshwa kwa njia za kitakwimu.

Huduma za Afya	Jamii ifaidikayo	Faida kwa watu binafsi		Jumla
		Wanawake	Wanaume	
Kukinga Maradhi				
Mafunzo ya Watumishi wa Afya				
Kuweka mazingira mazuri katika ofisi ya afisa afya wa wilaya (kama vile kutia uzio nk)				
Ujenzi wa kitengo kipya cha afya (wodi ya uzazi)				
Ununuzi wa madawa				
Kurusha vipindi vya redio				
Ushiriki katika siku za kitaifa na kimataifa (kama vile Siku ya Ukimwi Duniani)				
Ruzuku za watumishi				
Jumla ya waliopata huduma				

Nyenzo ya pili: Upembuzi wa Matumizi ya Jamii Yasiyozingatia Jinsia

Hii nyenzo stahilivu huonyesha kwa hakika utoaji wa huduma za jamii kuendana na jinsia. Inasaidia hasa kuweka msingi wa mifumo ya ufuatiliaji.

- Hii yahitaji kupima yafuatayo: i) gharama ya kutoa huduma, kama vile gharama ya kujenga shule ya msingi ndani ya mwaka mmoja; ii) idadi ya vitu vilivyotumiwa na wanaume, wanawake, wavulana na wasichana.

- Kujirudia kwa Manufaa, yaani 'Benefit incidence' kwaweza kupigiwa hesabu kama thamani ya matumizi ikizidishwa na idadi ya vitu vilivyotumiwa na watu. *Benefit incidence* hutegemea mambo yafuatayo:

    1. Mgawanyo wa matumizi katika kutoa huduma kwa umma

    2. Mwenendo wa kaya katika utumiaji wa huduma za umma

Nyenzo ya 3: Tathmini za Sera Zizingatiazo Masuala ya Jinsia / Tathmini ya Matumizi kwa Sekta

Hii hujumuisha kubainisha msababishano unaotarajiwa kutoka kwenye matumizi yaliyopangwa shughuli zinazokubaliwa, pamoja na matokeo yatazamiwayo, na athari za matokeo haya kwa wanaume na wanawake. Ni kama mchoro unaoonyesha hatua kwa hatua uhusiano au utaratibu wa vitu katika mfumo. Taarifa muhimu zaweza kupatikana kwa njia zifuatazo:

1. Maelezo juu ya matukio yatarajiwayo: Kwa mfano, ongezeko katika matumizi juu ya elimu linatarajiwa a) kuongeza idadi ya wasichana wanaoandikishwa shuleni (na kupunguza msigano wa kijinsia uliopo katika uingizaji wa watoto shule), na b) kuboresha viwango vya elimu kwa wasichana (na kupunguza msigano uliopo katika ubora wa viwango vya elimu kati ya wavulana na wasichana).
2. Mchoro wa kuonyesha mahusiano;
3. Orodha kaguzi ya maswali;
4. Muundo wa upembuzi ulioandaliwa kitabuni; na
5. Kutengeneza bajeti kwa kulenga utekelezaji wa programu.

Nyenzo ya 4: Utenganishaji wa Matumizi katika Makundi Yaendanayo na Jinsia

- Matumizi ya umma huchambuliwa:
  - Kwa wilaya na makundi ya kiutendaji
  - Kwa matumizi ya kawaida na ya majengo (mitambo)
  - Kwa mambo kama watumishi, vitendea kazi, mafuta ya magari nk.
- Hii hufanya iwe ngumu kutathmini kama matumizi ya umma yanaendana na mahitaji ya makundi mbalimbali ya wanaume na wanawake katika jamii; na hata jinsi makundi haya yanavyoweza kufaidika na matumizi haya.
- Aina nyingi za utenganishaji ugusao jinsia zaweza kufanyika na kuonyeshwa kwa njia ya jedwali na michoro. Kwa mfano:
  - Matumizi yalengayo usawa wa jinsia
  - Huduma zizingatiazo vipaumbele vya wanawake
  - Mfumo wa uendeshaji wa masuala ya jinsia wilayani
  - Kuhamisha mapato kwa kuzingatia vipaumbele vya wanawake
  - Kuwianisha jinsia katika sekta ya ajira
  - Kuwianisha jinsia katika utoaji wa misaada ya kibiashara
  - Kuwianisha jinsia katika mikataba ya sekta ya umma
  - Kupunguza kiwango cha msigano wa kijinsia

Nyenzo ya 5: Uchambuzi wa Uhusiano wa Bajeti na Matumizi ya Muda

Sehemu kubwa ya yafuatayo huhusiana zaidi na *gender budgeting* ngazi ya taifa. Hata hivyo ngazi hii yaweza kuboreshwa kwa kutumia taarifa zilizokusanywa ngazi ya wilaya na matokeo ya kazi zilizofanywa na uongozi wa kitaifa katika kusaidia ushirikishwaji ngazi za chini katika mchakato wa bajeti. Hatua ya kwanza ni kukusanya taarifa juu ya jinsi ya wanakaya wanavyoutumia muda wao. Taarifa juu ya matumizi ya muda, zilizogawanywa kwa kufuata umri na jinsia, zaweza kutumiwa kuonyesha mahusiano kati ya bajeti ya serikali na mipango ya wanakaya katika matumizi ya muda wao. Kwa mfano:

- Kutafuta kodi ya uzalishaji, yaani uwiano wa muda autumiao kuitumikia jamii katika shughuli za uzalishaji bila kulipwa. Mabadiliko kwenye kodi ya uzalishaji huhusiana kwa karibu sana na mabadiliko kwenye kodi nyinginezo.
- Kutafuta uwiano wa mchango na matokeo katika sekta za kijamii, huhusisha kazi za kutoa huduma bure kwa jamii kama mchango (input) na matokeo (output) na pia matumizi ya umma yafanywayo na sekta za kijamii.
- Kutafuta matumizi ya muda na fedha yafanywayo na kaya kwenye huduma kama vile afya, elimu, uchimbaji mitaro ya maji machafu, na usafirishaji. Mabadiliko kwenye matumizi ya muda yaweza kuhusishwa na mabadiliko kwenye matumizi ya umma.
- Kwa kujaribu kuipangia gharama kazi ifanywayo bila malipo, 'satelite account' yaweza kuundwa kwa nchi nzima ili kujua pato jumla la kazi iliyofanywa na kaya. Hii yaweza kusaidia watunga sera kubainisha uhusiano kati ya pato la

jumla la kaya na pato la jumla la taifa.

Nyenzo ya 6: Mfumo wa Kiuchumi wa Muda wa Wastani Uzingatiao Jinsia

Mifumo ya kiuchumi ya muda wa kati (au wastani) inayozingatia jinsia hujengwa kwa kutumia miundo ya kiuchumi kama vile:

1. Miundo ya kupangilia uchumi (financial programming models)
2. Uwiano wa kudumu (fixed coefficient)
3. Mifumo ya mahesabu izingatiayo msigano na ukuaji (gap, growth accounting models)
4. Mifumo mikubwa ya kiuchumi (macro-econometric models)
5. Mifumo linganifu (computable general equilibrium models)

Angalia: Kwa sasa nyenzo zote hapo juu hazizingatii muundo wa kijinsia.

SEHEMU YA 7: MTAZAMO WA PILI:

msisitizo juu ya kuijengea jamii uwezo

Mtazamo ufuatao waweza kutambulishwa kwa washiriki kwa njia ya warsha. Yaweza kuhitahijika masaa matatu mpaka matano.

7.1 Utangulizi

Muundo huu wa PETS ni nyenzo ya maana sana katika kuijengea jamii uwezo. Mchakato wake ni wa kivumbuzi, kwa sababu huwawezesha wanajamii kukusanya taarifa wanazohitaji, na kupokea tu maongozi au ushauri kutoka kwa wawezeshaji waliobobea. Husimamia mchakato wa bajeti kuanzia ngazi za chini mpaka za juu, na kukusanya taarifa kutoka ngazi ya jamii kulingana na mahitaji ya jamii husika.

Lengo la mtazamo huu ni kutoa kadi za kurekodia mafanikio. Kadi hizi Tanzania zimeitwa PIMA CARDS; kwingineko kadi hizi zinaitwa 'Community Score Cards.'

7.2 PIMA Card nini?

PIMA Card ni nyenzo rahisi ya kukusanya taarifa isaidiayo kujenga uwezo wa jamii kwa kuwawezesha wanajamii 'kuwa na kauli'. Huipa jamii muundo wa kukusanyia taarifa za kitakwimu na zile stahilifu juu ya viletwavyo (inputs), vitolewavyo (outputs) na matokeo ya huduma zitolewazo na serikali. Cha muhimu zaidi, jamii yenyewe ndiyo huamua sekta zipi zifuatiliwe. Taarifa hizi zaweza kutumika katika kikao cha pamoja (kama vile cha ujirani mwema) ili kukuza uwajibikaji. Zikitumika ipasavyo, PIMA cards zaweza kusaidia kujenga uwezo wa jamii.

Ifuatayo ni mifano ya PIMA card. Katika sehemu ya kwanza jamii imechagua kufuatilia ukarabati na utunzaji wa barabara na madaraja, na sehemu ya pili wamechagua kutazama kilimo.

PIMA Card: Mfano wa 1: Barabara

	Kiashirio			
1	Kudhibiti Umasikini			
	Ukarabati wa barabara kubwa, barabara ndogo na madaraja a. Je, kuna barabara kuu zozote, barabara ndogo au madaraja yoyote kijijini kwenu yaliyokarabatiwa ndani ya miezi 12 iliyopita? b. Kama jibu ni 'Ndiyo', taja majina ya barabara na madaraja yaliyokarabatiwa, taja urefu wa barabara uliokarabatiwa, na pia onyesha gharama iliyotumika.			Ndiyo/ Hapana
	Jina la barabara kubwa, barabara ndogo au daraja la barabara Urefu (Km) Gharama			
	1.			
	2.			
	3.			
2	Utengenezaji wa barabara kubwa, barabara ndogo na madaraja			
	a. Je, yamefanyika matengenezo yoyote kwenye barabara kubwa yoyote, barabara ndogo au daraja lolote la barabara iingiayo kijijini kwenu ndani ya miezi 12 iliyopita? b. Kama jibu ni 'Ndiyo', taja majina ya barabara na madaraja yaliyofanyiwa matengenezo, taja urefu wa barabara uliotengenezwa, na pia onyesha gharama iliyotumika.			Ndiyo/ Hapana
	Jina la barabara kubwa, barabara ndogo au daraja la barabara			
	1.			
	2.			
	3.			
3	Ujenzi wa barabara mpya na barabara ndogo ndogo			
	a. Je, kuna barabara yoyote mpya (kubwa au ndogo) iliyojengwa maeneo yenu ndani ya miezi 12 iliyopita? a. Kama jibu ni 'Ndiv yo', taja majina ya barabara hizi na urefu wake. Taja pia kiasi cha fedha kilichotumika kujenga barabara hizi.			Ndiyo/ Hapana
4	Jina la barabara kubwa, barabara ndogo Urefu (Km) Gharama			
	1.			
	2.			Ndiyo/Hapana
	3.			
	Ujenzi wa madaraja mapya na makalvati			
	a. Je, kuna madaraja yoyote au makalvati mapya yaliyojengwa maeneo yenu ndani ya miezi 12 iliyopita? b. Kama jibu ni 'Ndiyo' taja majina ya madaraja na makalvati, na gharama zake.			
	Jina la daraja au kalvati Gharama			
	1.			
	2.			
	3.			
5	Kuna suala gani jingine ambalo jamii yako ingependa kulishughulikia kuhusiana na barabara?			

PIMA Card: Mfano wa 2: Kilimo na Masoko

<table>
<tr><td colspan="6">Kilimo na Masoko " Vichocheo vya Uzalishaji"</td></tr>
<tr><td>B1.</td><td colspan="5">Ushauri wa Kitaalam</td></tr>
<tr><td>B1.1</td><td colspan="5">Aina gani za ushauri zilitolewa kijijini kwenu mwaka uliopita? Uliridhika kiasi gani na huduma hizi?</td></tr>
<tr><td rowspan="14"></td><td rowspan="14">Kudhibiti wadudu waharibifu
Mbegu bora zaidi
Ushauri juu ya Mazao yanayozaa sana
Ushauri wa jinsi ya kusindika mazao
Huduma za mifugo
Kilimo kinachozingatia utunzaji wa mazingira
Kuhifadhi ardhi
Kuanzisha vyama vya wakulima
Mbinu za umwagiliaji
Utunzaji wa mazao
Kusindika mazao
Kusindika mazao ya mifugo</td><td>Hakuna Huduma</td><td>Duni</td><td>Ya kuridhisha</td><td>Nzuri</td></tr>
<tr><td></td><td></td><td></td><td></td></tr>
<tr><td></td><td></td><td></td><td></td></tr>
<tr><td></td><td></td><td></td><td></td></tr>
<tr><td></td><td></td><td></td><td></td></tr>
<tr><td></td><td></td><td></td><td></td></tr>
<tr><td></td><td></td><td></td><td></td></tr>
<tr><td></td><td></td><td></td><td></td></tr>
<tr><td></td><td></td><td></td><td></td></tr>
<tr><td></td><td></td><td></td><td></td></tr>
<tr><td></td><td></td><td></td><td></td></tr>
<tr><td></td><td></td><td></td><td></td></tr>
<tr><td></td><td></td><td></td><td></td></tr>
<tr><td></td><td></td><td></td><td></td></tr>
<tr><td>B1.2</td><td>Naridhishwa na huduma za ushauri wa masuala ya kilimo zitolewazo</td><td colspan="4">Nakubali sana
Nakubali
Sina hakika
Sikubaliani hata kidogo</td></tr>
<tr><td>B1.3</td><td>Ni zipi kati ya aina hizi 5 za ushauri unadhani zinahitajika sana na walimu kwenye jamii yenu?</td><td colspan="4">1.
2.
3.
4.
5.</td></tr>
</table>

7.3 PIMA Cards zaweza kutumiwaje?

PIMA card ni nyenzo rahisi kwa kufanyia tathmini, ambayo imelengwa kurahisisha mawasiliano. Umalizapo kutumia kadi hizi kukusanya taarifa, kadi hizi zaweza kutumiwa tena baadaye ili kusimamia na kuangalia kwa karibu mwenendo wa viashirio mbalimbali.

Kadi hizi zaweza pia kutumiwa kwa njia nyingi tofauti kulingana na matakwa na mahitaji ya jumuiya husika kama vile:

- Kupima mwenendo wa vipaumbele vya jamii juu ya MKUKUTA au shughuli nyinginezo za maendeleo kama vile upatikanaji wa maji salama kwa akinamama wa vijijini, na huduma za kilimo.
- Kufuatilia bajeti za serikali kwenye masuala ya huduma za kilimo, elimu, afya, maji na barabara.
- Kutathmini kilichokwishafanyika au kukamilishwa katika jamii kutokana na bajeti.
- Kutathmini mwenendo wa uboreshaji wa maisha kwa kutumia viashirio vya MKUKUTA.

7.4 Umuhimu wa PIMA Cards

Jamii ambazo tayari zina uwezo wa kujiwekea vipaumbele vya mahitaji yao na kukusanya taarifa kutumia PIMA cards zaweza kuchambua na kutafakari taarifa walizokusanya na kuazimia cha kufanya ili kusonga mbele.

Mashirika ya kijamii yana jukumu la kusaidia jamii ziweze kufanya kazi kwa maelewano na ukaribu zaidi na serikali za mitaa. Katika ngazi ya taifa pia zaweza kusaidia kwa kuchangia kutoa taarifa kwa Mfumo wa Serikali wa Kudhibiti Umasikini ili kuchangia katika uandaaji wa sera zinazolenga kuwasaidia wasio na uwezo.

Katika ngazi ya jamii PIMA Cards zaweza kuonyesha:

- Jinsi bajeti zinavyoweza kutumika kuleta matokeo
- Kiwango ambacho jamii huridhishwa na matokeo ya bajeti
- Jinsi serikali za mitaa zinavyojishughulisha na vipaumbele vya jamii
- Gharama zilizofichika au mianya (ya rushwa)
- Ubora wa maisha ya wanajamii

7.5 Vichocheo vya mafanikio ya PIMA Cards

Jamii zinapaswa kuelewa vema mazingira ambayo kwayo watafanya ufuatiliaji. Ni vema kuwa na vipaumbele kama vile nia ya kudhibiti umasikini, sera zinazolenga kusaidia wasio na uwezo kama vile MKUKUTA, sababu na viashirio vya umasikini, na malengo ya kupunguza umasikini.

Kwa uelewa huu jamii zitaweza kutathmini mwenendo wa juhudi za kupunguza umasikini kwa kufuatilia bajeti za vijiji na wilaya na shughuli zinazolengwa kutekelezwa kwa bajeti hizi, na hatimaye matokeo ya shughuli zenyewe. Ni muhimu sana kwa wawezeshaji kuwa na uelewa wa kutosha ili kuhakikisha kwamba jamii zinawezeshwa kukusanya taarifa sahihi na kufanya maamuzi sahihi juu ya hatua za pamoja.

PIMA Cards hazipaswi kutumiwa kama nyenzo ya kutumia mara moja tu, ila kama nyenzo ya udhibiti inayopaswa kutumiwa mara kwa mara kama ilivyo PETS.

Hofu ya jamii kukataliwa maombi yao na maafisa wa juu inapaswa ipunguzwe na mchango wa mashirika ya kijamii ambayo hupaswa kuwa kiungo na mpatanishi. Lakini upatanishi huu pia unapaswa kufanywa kwa uangalifu sana. Tukizitazama PIMA Cards sambamba na PETS (kama ilivyoelezwa kwenye mwongozo huu), PIMA Cards zinajenga mazingira ambapo viongozi wa serikali za mitaa, madiwani na jamii nzima wanaweza kufaidi huduma bora zaidi za serikali yao.

Kama ilivyo kwenye methodolojia zote za PETS, ufuatiliaji unapaswa kutazamwa kama shughuli shirikishi inayohusisha washiriki wengi katika jamii.

Mchoro X huonyesha aina ya shughuli na michakato inayoweza kuboreshwa na PIMA Card:

Mchoro: Shughuli za PIMA Card



Mchoro: Hatua za Kufuata ukitumia PIMA Cards

7.6 Mchakato wa PIMA Card



Mchoro: Hatua za Kufuata ukitumia PIMA Cards

7.7 Shughuli za PIMA Cards: Hatua kwa Hatua

HATUA YA KWANZA: Matayarisho Ngazi ya Wilaya

1. Fanya warsha ya kupanga mikakati ngazi ya wilaya ikiwahusisha viongozi wa serikali za mitaa, madiwani, mashirika ya kijamii na wawakilishi wa jamii shiriki katika ufuatiliaji. Lengo la mkutano huu ni kuzielezea PETS na PIMA Cards ili watendaji waweze kupata imani na ushirikiano wa wahusika wote. Hii yaweza pia kuwa sehemu ya warsha ya utangulizi.

2. Yawezekana pia kufanya makubaliano na watumishi wa serikali za mitaa juu ya utoaji wa habari za mipango na bajeti (mara kwa mara au kila baada ya miezi mitatu) katika muundo utakaokubaliwa. Baada ya makubaliano haya taarifa husika zaweza kuanza kutolewa kwa jamii nzima.

HATUA YA PILI: Matayarisho Ngazi ya Jamii

1. Fanya mkutano wa hadhara katika kila jamii ihusikayo na ufuatiliaji ili kujadili:

    - Sababu na maana ya umasikini.
    - Jinsi ya kujua kama umasikini umepungua.
    - Mikakati ya kupunguza umasikini, malengo, viashirio na shughuli husika. Tumia MKUKUTA kama muktadha.
    - Malengo na faida za PETS kwa jumla, hasa PIMA Cards.

1. Wakati wa mkutano jamii iwezeshwe ili kuamua:

    - Sekta zistahilizo kipaumbele katika kupunguza umasikini (baada ya majadiliano katika makundi ya wanaume, wanawake, vijana, wasiojiweza, wazee na watoto)
    - Sekta ambazo jamii ingependa kufuatilia, kama vile afya, elimu, maji na barabara.
    - Wajumbe wa kamati watakaoshiriki katika ukusanyaji wa taarifa kwa PIMA Cards. Kamati itakuwa na watu 7 hadi 15 na ni muhimu kwamba sehemu kubwa ya jamii iwakilishwe katika kamati hii.

HATUA YA TATU: Jua juu ya Viingiavyo (inputs) – Bajeti za Serikali za Mitaa

1. Pata Bajeti ya Serikali za Mitaa juu ya sekta ambazo jamii ingependa kufuatilia, kama vile Elimu, Afya, Kilimo, Maji, Barabara, nk.
2. Chambua bajeti iliyotengwa kwa ajili ya shughuli za MKUKUTA
3. Tengeneza jedwali la bajeti kwa kila shughuli ya mkukuta iliyoonyeshwa kwenye bajeti.

[Nyenzo ya kwanza (hapa chini) yaweza kutumiwa kwa shughuli hii, pamoja na fomu iliyotolewa yaweza kusaidia kupata taarifa (ambazo hazijafanyiwa upembuzi) kutoka ngazi ya wilaya.]

HATUA YA NNE: Andaa PIMA Card kwa Kila Sekta

Hii itahusisha maswali juu ya:

1. Shughuli za MKUKUTA zilizotengewa bajeti. Mfano, vyumba vingapi vya madarasa vimejengwa ndani ya miezi 12 iliyopita?
2. Shughuli za kipaumbele ambazo hazikutengewa bajeti. Kwa mfano, jamii huchukua hatua gani kulinda vyanzo vya maji?

3. Vyanzo vinginevyo ambavyo ni muhimu kwa jamii.

Andaa PIMA Card kwa kila sekta ili ijazwe na maafisa husika wa serikali za mitaa ngazi ya wilaya. Kadi hii inapaswa kuulizia juu ya shughuli na matumizi katika sekta husika katika ngazi ya wilaya.

[Tumia nyenzo 2 (chini) juu ya utengenezaji wa PIMA card]

HATUA YA TANO: Kusanya Taarifa kutumia PIMA Cards

1. Toa mafunzo kwa kamati moja juu ya kutumia PIMA Card na uijaribu kadi hii katika jamii husika.
2. Fanya mabadiliko yoyote yanayostahili.
3. Toa mafunzo kwa kamati nyinginezo.
4. Saidia kamati kukusanya taarifa. Hakikisha pia kamati inapangiwa muda maalum wa kumaliza kukusanya taarifa.
5. Chunguza taarifa zilizokusanywa na (kama kuna mapungufu kwenye taarifa hizi) pata taarifa sahihi kutoka kwenye jamii.
6. Baada ya kumaliza kutumia PIMA Card itisha mkutano wa hadhara kusambaza taarifa zilizokusanywa.

HATUA YA SITA: Kuandika Ripoti na Mrejesho

1. Andaa rasimu ya ripoti ihusishayo taarifa kutoka wilayani na uzoefu wa jamii
2. Omba watu wengine waikague ripoti yako
3. Peleka taarifa (mrejesho) kwenye jamii
4. Peleka taarifa (mrejesho) kwenye Serikali za Mitaa
5. Andaa mkutano kati ya jamii na Serikali za Mitaa ili:
    - Kujadili taarifa
    - Kuazimia juu ya hatua stahili kufuatilia vipaumbele vya jamii
    - Kuangalia jinsi ya kuendelea na ushirikishanaji wa taarifa na mwitiko hatua kwa hatua.

Mchoro ufuatao huonyesha hatua zilizofuatwa



7.8 Nyenzo maalum na Mazoezi ya Kufundishia

7.8.1 Nyenzo ya Kwanza: Uchambuzi wa Bajeti

Unapokuwa na nyaraka za bajeti kutoka kwa mamlaka za wilaya, ambazo waweza kuwa umezipata kutokana na fomu iliyokwishaelezwa (ukurasa….), unahitaji kuzichunguza taarifa na kuichambua bajeti. Kwanza angalia utofauti kati ya bajeti ya matumizi ya kawaida na bajeti ya maendeleo:

Uchambuzi wa Bajeti

1. Bajeti ya Matumizi ya Kawaida
- Mishahara, magari, tarakilishi (kompyuta) nk.

2. Bajeti ya Maendeleo

Huhusisha michango juu ya shughuli za MKUKUTA kama vile:

- Ukuzaji wa kilimo
- Mafunzo ya Walimu
- Kukuza uelewa wa masuala ya UKIMWI
- Ujenzi/ukarabati wa vyanzo vya maji

Katika Bajeti ya Maendeleo:

1. Angalia fedha iliyotengwa kwa ajili ya shughuli za MKUKUTA
2. Kama kuna fedha iliyotengwa, hii ndiyo utakayohitaji kufuatilia. Kwa mfano, kwa ujenzi wa vyumba vya madarasa.
3. Kama fedha kutoka kwa wafadhili ni sehemu ya bajeti, nani anayesimamia mradi uliopo? Serikali au mfadhili?
4. Kama hakuna fedha iliyotengwa kwa ajili ya shughuli yoyote ya MKUKUTA. Kwa mfano, kuhamasisha utunzaji wa maji, uliza serikali kwa nini hakukutengwa chochote kwa shughuli hii.

Kazi ya Kundi 1: Chambua Bajeti kwa Kufuata Sekta za MKUKUTA

1. Chunguza bajeti kwa ajili ya sekta iliyotajwa.
2. Orodhesha matatizo yoyote uliyobaini kwenye bajeti: kwa mfano vichwa vya habari haviendani na shughuli za MKUKUTA. Utalazimika kukagua kila ukurasa.
3. Kwa kila sekta utakayofuatilia, andaa jedwali la bajeti kwa shughuli zote za MKUKUTA (tazama hapa chini). Angalia maelezo yoyote ya kina katika bajeti kama vile, angalia shughuli zinazotekelezwa kati ya zile zilizotengewa fedha kwenye bajeti.

Wasilisha ulichogundua

Jedwali la Bajeti ya Elimu – Wilaya X

Shughuli ya MKUKUTA	**Iko katika Bajeti**	**Haiko katika Bajeti**	**Kiasi Kilichotengwa**	**Maelezo Mengineyo (kama majina ya sehemu nk)**
Mafunzo kwa Waalimu				
Kujenga Madarasa Mapya				
Samani				
Kuimarisha Ukaguzi wa Mashule				

Kazi ya Kundi 2: Andaa PIMA Card kwa ajili ya Jamii

Kwa sasa tayari unao mgawanyo wa bajeti juu ya shughuli za MKUKUTA kwa kila sekta unayofuatilia katika kipindi uliojipangia.

Ni maswali gani utauliza katika PIMA Card?

Andaa maswali kwa yafuatayo:

- Shughuli iliyotengewa fedha katika sekta unayofuatilia ni ipi? Kwa mfano: kujenga madarasa mawili na nyumba ya mwalimu)
- Rasilimali gani ililetwa kwa ajili ya shughuli hii?
- Fedha (au rasilimali kwa ujumla) zilitoka wapi?
- Ni fedha au rasilimali zipi hasa zilitumika kwa shughuli hii?
- Je, jamii inaridhirishwa na matokeo ya shughuli hii? Toa sababu.
  1. Je, shughuli za MKUKUTA ambazo hazikutengewa fedha kwenye bajeti ya wilaya (kama vile zana za kufundishia, vitabu vya kiada nk) zinagharimiwa namna gani?
  1. Masuala mengine muhimu kwa jamii:
- Jamii yako ina matatizo gani mengine juu ya elimu ya msingi?
- Taja masuala (matatizo) haya ukiyapanga kufuatana na umuhimu wa kila moja.

7.8.2 NYENZO YA PILI: Kulinganisha Mitazamo Ngazi za Wilaya na za Jamii

Njia mojawapo ya kutumia kadi PIMA na usimamizi ufanywao katika ngazi ya jumuiya ni kuitumia pamoja na taarifa za kutoka ngazi ya wilaya. Kikao cha kupeana taarifa za utekelezaji wa maamuzi chaweza kutumika kuwakutanisha wawakilishi wa ngazi za jumuiya na wilaya ili kubadilishana mitazamo na kutafakari mitazamo hii kwa nia ya kuboresha bajeti na mchakato mzima wa mipango, na matokeo yake.

Maafisa husika wa wilaya wanaweza kuombwa kujaza fomu ya kujitathmini ambayo huashiria maswali ambayo yataulizwa na timu ya usimamizi ngazi ya jumuiya. Mfano wa fomu ni huu hapa chini:

Kilimo na Masoko: Kadi ya Kujitathmini (Ngazi ya Wilaya)	
A	Uzalishaji wa Mazao
A1	Ubora wa Mazao ya Biashara Ni kiasi kipi cha mazao ya biashara kilizalishwa katika wilaya yenu kwa kila mmoja wa miaka mitatu iliyopita? Zao 2002 2003 2004 Ongezeko au Upungufu Sababu zipi zilifanya kuwa na ongezeko au upungufu?
A2	Ni mazao yapi ya biashara yamekuwa yakilimwa wilayani kwenu tangu mwaka jana?
A3	Ubora wa Mazao ya Biashara a. Je, ubora wa mazao ya biashara yazalishwayo wilayani kwenu umeongezeka, kupungua au hakukuwa na badiliko lolote? Zao 2002 2003 2004 Ongezeko au Upungufu Sababu zipi zilifanya kuwe na ongezeko au upungufu?
A4	Mazao kwa ekari Kuna kiasi gani cha mazao ya biashara na mazao makuu ya chakula mlichozalisha wilayani kwa kila ekari? Zao 2002 2003 2004 Ongezeko au Upungufu Je, kuna sababu zipi kwa ongezeko au upungufu?
A5	Mifugo Kwa makadirio, ni idadi gani ya kila moja ya aina zifuatazo za mifugo ilikuwa wilayani mwako kwa miaka iliyotajwa? Zao 2003, 2004 na 2005 Ongezeko au Upungufu Ng'ombe Mbuzi Kondoo
B.	Maswali ya Jumla
B1	Tafadhali orodhesa kwa kufuata ukubwa, matatizo sugu matano yanayosibu uzalishaji wa mazao na mifugo wilayani kwenu. 1. 2. 3. 4. 5.

B2	Tafadhali orodhesha kwa kufuata ukubwa, matatizo matano sugu yanayosibu uuzaji wa mifugo na mazao ya shamba wilayani kwenu. 1. 2. 3. 4. 5.
C.	Huduma za Ushauri wa Kitaalam katika Kilimo
C1	Kati ya Julai 2004 na Juni 2005 ni katika jamii zipi wataalamu wa kilimo walitoa mafunzo au taarifa muhimu au msaada juu ya mambo ya kilimo yafuatayo? Kudhibiti wadudu waharibifu Kutoa mbegu bora Ushauri wa kupanda mazao yanayozaa zaidi Vyombo vya kusindika mazao Huduma za mifugo Tekinolojia ya kutumia ardhi bila kuathiri mazingira Kuhifadhi ardhi Uanzishaji wa vyama vya ushirika vya wakulima Njia za umwagiliaji Kuhifadhi mazao Kusindika mazao Kusindika mazao ya mifugo
C2	Kati ya Julai 2004 na Juni 2005 ulichanja ng'ombe wapi, lini na ulitumia fedha kiasi gani? Wapi, lini na kiasi gani cha fedha kilitumika? 1. 2. 3. 4. 5. 6.
D	Vyanzo vya Maji
D1	Je, kuna vyanzo vyovyote vya maji (mabomba, umwagiliaji mdogo mdogo, umwagiliaji wa asili, vidimbwi nk) vilivyoanzishwa au kufanyiwa ukarabati kati ya Julai 2004 na Juni 2005? Taja aina ya chanzo cha maji, kilipo na kiasi cha fedha kilichotumika
E	Barabara
E1	Je, wilayani kwako kuna barabara yoyote kuu au ndogo, ama hata daraja lililofanyiwa ukarabati au kujengwa kati ya Julai 2004 na Juni 2005? Taja jina la barabara au urefu wake Barabara ndogo katika kata au daraja: kiwango cha fedha (Tsh/=) 1. 2. 3. 4. 5. 6. 7. 8.

SEHEMU YA 8: Hitimisho

8.1 kutoka kujenga mifumo hadi kufanya mabadiliko hasa yapatikane

Hapo mwanzo tuliongelea *constructive engagement* kama muundo wa ushawishi katika uanzishaji wa PETS. Hii ni sehemu tu ya mchakato wa kujenga mifumo ya kuwezesha mabadiliko ya kudumu yatokee. Kwa kupitia taarifa ambazo PETS husambaza, kwaweza kuwa na mwanya wa ushawishi katika mabadiliko ya bajeti, kama vile katika utengaji au utoaji wa pesa kutekeleza jukumu ambalo wanajamii wameona lina manufaa kwao. Mifano zaidi yaweza kuwa uongezaji wa pesa ngazi ya vijiji badala ya wilayani, au upangaji wa matumizi unaozingatia kutekeleza kwa usawa mahitaji ya wanaume na wanawake.

Ili kufanikisha mabadiliko ya namna hii, baadhi ya hatua muhimu za kufuata ni:

- **Kuweka bayana ujumbe:** Nini hasa unachotaka kutekeleza? Je, una ushahidi tosha ili kuwashawishi walengwa?
- **Kuchanganua oganaizesheni yenu:** Bainisha uwezo na mapungufu yenu. Je, kuna mianya na vikwazo vipi vinavyowakabili katika kufanya ushawishi juu ya suala hili? Je, mnazo rasilimali zote zinazohitajika – yaani watu na fedha?
- **Kupanga mipango shirikishi** ili kupata wadau wengi iwezekanavyo kushiriki katika mkakati wa ushawishi. Hii yaweza kuwa sehemu ya kikao cha mrejesho kilichotajwa katika kipengele 3.4.
- **Kuweka malengo bayana**: Weka malengo kulingana na ujumbe wa jumla ulionao, kisha yagawe malengo haya katika vijisehemu vidogo vidogo ili yatekelezeke kirahisi.
- **Kujijengea marafiki** ili ujipe hakika ya kupata rasilimali na msaada zaidi kama itahitajika. Vyombo vya habari vyaweza kuwa muhimu sana hatua hii. Je, wawezaje kuwashirikisha kwa karibu waandishi wa habari? Njia mojawapo ni kuwashirikisha tangu mwanzo katika kile unachofanya, kuanzia kwenye warsha za mwanzo na mafunzo ili nao waielewe vema PETS.
- **Kusimamia na kutathmini** unachofanya kwa kila hatua unayopiga. Tathmini mabadiliko kila yaanzapo kujitokeza. Kuwa tayari kupokea mawazo na mitazamo mipya kwani yaweza kuchangia kuleta mabadiliko yanayotarajiwa. Ukishafanikiwa (au kushindwa!) fanya upembuzi yakinifu uone kama kuna ulichofanya ambacho kilikuwa bora (au hafifu). Jifunze kutokana na ulichoona ili ufanye vema (vema zaidi) safari nyingine. Shirikisha wenzio ulichojifunza.

8.2 Habari za nyongeza

Kama ilivyoelezwa katika mwongozo huu, PETS yaweza kuwa njia bora sana ya kuyaelezea matatizo mengi yanayowasibu maafisa ngazi ya wilaya, madiwani na mashirika yasiyo ya kiserikali katika shughuli zao za kila siku. PETS hufunua taarifa za masuala ya kifedha ili kuwezesha uelewa na hatimaye ushiriki wa wananchi. Hii humfaidisha kila mtu katika jamii kwani rasilimali zitatumiwa vema zaidi ili kutekeleza malengo ya MKUKUTA. Lakini hasa,

- Mashirika yasiyo ya kiserikali yataweza kuchukuwa nafasi kubwa zaidi katika kukuza na kuimarisha mtiririko wa taarifa baina ya jamii na uongozi wa

wilaya,

- Madiwani watakuwa na nafasi nzuri pia, hasa kutokana na kutambua hali halisi ilivyo katika maeneo wanayowakilisha, na jinsi huduma za serikali za mitaa zinavyokidhi mahitaji ya wananchi,
- Maafisa wa wilaya wataweza kutenga na kutumia fedha kwa uangalifu zaidi.
- Madiwani na maafisa wilaya kwa pamoja wanaweza kupata kibali zaidi machoni mwa wananchi kutokana na huduma yao kwa jamii wanazoongoza.
- Wilaya kwa jumla itakuwa kwenye nafasi bora sasa kuomba msaada serikali kuu, kwa kuwa sasa watakuwa wanajuwa vema na kwa hakika zaidi mahitaji halisi kuliko ilivyokuwa hapo nyuma. Watakuwa pia wanajua chanzo na ukubwa wa matatizo katika sekta tofauti tofauti na jamii tofauti tofauti.

Tunataraji kwamba mwongozo huu utawasaidia watu na makundi tofauti kuanzisha PETS. Kwa kuwa hii si kazi kamilifu katika hatua hii, tafadhali usisite kuwasiliana na mashirika yafuatayo ili kupata taarifa au msaada zaidi. Kama una maoni juu ya jinsi ya kuuboresha mwongozo huu tafadhali usisite kutushirikisha. Tutafurahi sana kusikia chochote kutoka kwako.

- ❖ Hakikazi Catalyst
- ❖ NGO Policy Forum (Baraza la Sera la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali)
- ❖ REPOA (Utafiti juu ya Kupunguza Umasikini)
- ❖ TGNP (Mtandao wa Jinsia Tanzania)

Kiambatisho 1: Vyanzo zaidi vya Kujisomea

Tovuti ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ina habari nyingi kuhusu mambo ya maendeleo. Waweza kupata nakala za Kiswahili na Kiingereza za Dira 2025, MKUKUTA, MKUKUTA Monitoring Master Plan kwenye http://www.tzonline.org. Baadhi ya machapisho haya yanapatikana katika lugha rahisi zaidi kutoka Hakikazi.

Tovuti za mashirika yaliyoshiriki ni:

http://www.repoa.or.tz
http://www.tgnp.org
http://www.hakikazi.org
http://www.policyforum.or.tz

Magnus Lindelow (2002) Holding Governments to Account: Public Expenditure Analysis for Advocacy, Save the Children, London

Oxfam / TEN/MET/ Kate Dyer (2003) A Simple Guide to Working with Finances and Education (iko pia kwenye tovuti ya *International Budget Project*)

Miongoni mwa taarifa muhimu za kimataifa ni:

The International Budget Project: http://www.internationalbudget.org

Institute for a Democratic Alternative in South Africa (IDASA) "who do?? a lot of budget work, including in Tanzania: : http://www.idasa.org

Kiambatisho 2: Fomu tupu ya PETS

SEKTA	Kilichopangwa	Kilichopokelewa	Kilichotumika makao makuu ya Halmashauri	Kilichohamishwa kupelekwa vijijini		Baki
				Kilichopangwa	Kilichopelekwa	
ELIMU						
Matumizi Mengine						
Ruzuku ya Mtu Mzima (kodi ya kichwa)						
Msaada wa Maendeleo						
Msaada wa Kujenga Uwezo						
Mapato ya Halmashauri						
Jumla						
AFYA						
Matumizi Mengine						
Maendeleo						
CHF						
Mapato ya Halmashauri						
Jumla						
BARABARA						
Mfuko wa Barabara						
Mapato ya Halmashauri						
Jumla						
KILIMO NA MIFUGO						
Matumizi Mengine						

DADP						
PADEP						
Mapato ya Halmashauri						
Jumla						
KAZI						
Matumizi Mengine						
Maendeleo						
Mapato ya Halmashauri						
Jumla						
MAJI						
Matumizi Mengine						
Maendeleo						
Mapato ya Halmashauri						
Jumla						
Maalum						
LGCDG						
LGDG						
Mapato ya Halmashauri						
Jumla						

[1] SNV (hakuna tarehe): Public Expenditure Tracking (PET) in Tanzania at district-level: effects on local accountability.

[2] Hata hivyo ni muhimu kujua kwamba uvujaji siyo lazima utokane na ufujaji au rushwa. Wakati mwingine fedha hutumika kufanya kitu kingine ambacho hakikuwa kimekusudiwa. Mfano ni kutumia fedha ngazi ya wilaya kununua mafuta ya gari / pikipiki ya mkaguzi wa mashule badala ya kupeleka fedha mashuleni.

[3] Kwaweza kuwa na haja ya kuwa na nakala ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wakati wa mafunzo ili kuwaonyesha washiriki vipengele husika.

[4] Haki ya kupata elimu hutambuliwa na Mapatano ya Umoja wa Mataifa juu ya Haki za Binadamu, na Mapatano juu ya Haki za Mtoto. Mtazamo tulionao ni kwamba mtoto ana haki hii, na kwamba serikali ina jukumu la kuhakikisha mtoto anapata haki hii. Lakini nchi nyingi haziwezi kumudu jukumu hili.

Kimeandaliwa na:
Hakikazi Catalyst
REPOA
TGNP

Kimehaririwa na kuchapishwa na Kikundi Kazi cha Serikali za Mitaa cha Policy Forum

© Policy Forum